# BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

**RIPOTI YA KAMATI YA KUDUMU YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**
**YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR**
**KWA MWAKA WA FEDHA 2024/2025**

**FEBRUARI, 2025**

## Contents


1. UTANGULIZI ........ 1

2. MADHUMUNI YA RIPOTI ........ 5

3. UCHAMBUZI WA KANUNI ........ 10

3.1 KANUNI YA WAHASIBU NA WASHAURI ELEKEZI ZANZIBAR, 2023 ........ 10

3.1.1 Makosa ya Uandishi ........ 10

3.1.2 Makosa ya Kimantiki ........ 11

3.1.3 Mapendekezo ........ 12

3.2 KANUNI ZA JUMLA ZA WATU WENYE ULEMAVU, 2023 ........ 13

3.2.1 Makosa ya Kiuandishi ........ 13

3.2.2 Makosa ya Kimantiki ........ 14

3.2.3 Mapendekezo; ........ 14

3.3 KANUNI ZA MAUZO WA MKOPO, 2023 ........ 15

3.3.1 Makosa ya Kimantiki. ........ 15

3.3.2 Makosa ya Kiundishi. ........ 15

3.3.3 Mapendekezo ........ 16

3.4 KANUNI ZA KAMISHENI YA ARDHI (ADA NA TOZO ZA ARDHI), 2024 ........ 17

3.4.1 Makosa ya Kiuandishi ........ 17

3.4.2 Makosa ya Kimantiki ........ 18

3.4.3 Mapendekezo ........ 19

3.5 KANUNI ZA UENDESHAJI WA MASOKO NA MAENEO YA BIASHARA KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA 2023 ........ 20

3.5.1 Makosa ya Kiuandishi. ........ 20

3.5.2 Makosa ya Kimantiki. ........ 21

3.5.3 Mapendekezo ........ 22

3.6 KANUNI ZA KUMALIZA MAKOSA, 2023 ........ 23

3.6.1 Makosa ya Kimantiki. ........ 23

3.6.2 Makosa ya Kiuandishi. ........ 24

3.6.3 Mapendekezo ........ 25
3.7 KANUNI ZA MASUALA YA DIASPORA (USAJILI WA DIASPORA), 2023. ........ 26
3.7.1 Makosa ya Kiuandishi. ........ 26
3.7.2 Makosa ya Kimantiki. ........ 27
3.7.3 Mapendekezo ........ 28
3.8 KANUNI YA BIDHAA CHAKAVU, 2023 ........ 29
3.8.1 Makosa ya Kiuandishi ........ 29
3.8.2 Makosa ya Kimantiki ........ 29
3.8.3 Mapendekezo ........ 31
3.9 KANUNI ZA JUMLA ZA MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR, 2023. ........ 32
3.9.1 Makosa ya Kiuandishi. ........ 32
3.9.2 Makosa ya Kimantiki ........ 33
3.9.3 Mapendekezo ........ 34
3.10 KANUNI YA KUCHUA WANAFUNZI WA VITENDO 2023 ........ 35
3.10.1 Makosa ya Kiuandishi ........ 35
3.10.2 Makosa ya Kimantiki ........ 35
3.10.3 Mapendekezo ........ 36
3.11 KANUNI ZA MAOMBI YA BARUA MAALIMU YA UTAMBUZI KWA WAFANYAKAZI 2023 ........ 37
3.11.1 Makosa ya Kiuandishi: ........ 37
3.11.2 Makosa ya Kimantiki ........ 38
3.11.3 Mapendekezo ........ 39
3.12 KANUNI ZA UTOAJI VIBALI KWA MAFUNDI WA UMEME,2023 ........ 40
3.12.1 Makosa ya Kiuandishi ........ 40
3.12.2 Makosa ya Kimantiki ........ 41
3.12.3 Mapendekezo ........ 42
3.13 KANUNI ZA MAONESHO NA MATAMASHA YA BIASHARA YA 2023 ........ 43
3.13.1 Mapendekezo ........ 44

3.14 KANUNI ZA USALAMA WA MAZAO YA CHAKULA ..... 45
3.14.1 Makosa ya Kiuandishi. ..... 45
3.14.2 Makosa ya Kimantiki ..... 45
3.14.3 Mapendekezo ..... 49
3.15 Kanuni za Utumishi Wa Umma (Usimamizi Wa Uhamisho Kwa Watumishi Wa Umma Wanaohamishwa Kikazi Nje Ya Utumishi Wa Zanzibar), 2024 ..... 50
3.15.1 Makosa ya Uandishi ..... 50
3.15.2 Makosa ya Kimantiki ..... 52
3.15.3 Mapendekezo ..... 53
4. HITIMISHO ..... 54
5. VIAMBATANISHO ..... 57
5.1 KIAMBATANISHO NAMBARI 1 ..... 57
5.2 KIAMBATANISHO NAMBARI 2 ..... 60
5.3 KIAMBATANISHO NAMBARI 3 ..... 64
5.4 KIAMBATANISHO NAMBARI 4 ..... 67
5.5 KIAMBATANISHO NAMBARI 5 ..... 71
5.6 KIAMBATANISHO NAMBARI 6 ..... 77
5.7 KIAMBATANISHO NAMBARI 7 ..... 80
5.8 KIAMBATANISHO NAMBARI 8 ..... 84
5.9 KIAMBATANISHO NAMBARI 9 ..... 88
5.10 KIAMBATANISHO NAMBARI 10 ..... 91
5.11 KIAMBATANISHO NAMBARI 11 ..... 93
5.12 KIAMBATANISHO NAMBARI 12 ..... 96
5.13 KIAMBATANISHO NAMBARI 13 ..... 98
5.14 KIAMBATANISHO NAMBARI 14 ..... 104

## RIPOTI YA KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO YA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR YA MWAKA 2024/2025

## 1. UTANGULIZI

Ni wajibu wangu kuanza kwa kutanguliza shukurani zangu kwa Allah (S.W) aliyetujaalia pumzi na afya na kutuwezeha kutimiza majukumu yetu kwa lengo la kuitumikia nchi yetu na watu wake na kutuwezesha kutimiza malengo ya Serikali yetu. Aidha Naomba kutumia fursa hii adhimu Kumshukuru Mhe, DK, Hussein Ali Mwinyi, Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, kwa kuendelea kuiongoza vyema Zanzibar na kutuletea maendeleo ambayo kila mzanzibari anajionea mwenyewe namna nchi inavyopiga hatua.

Vile vile, shukrani zangu nazielekeza kwako Mheshimiwa Spika na Viongozi wenziwe wa Baraza kwa uhodari na umakini wa hali ya juu walionao katika kuliongoza Baraza na wanavyotoa mashirikiano ya dhati kwa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo na kuiwezesha kutekeleza majukumu yake ipasavyo.

Pia sitoweza kuendelea pasi na kuwashukuru wajumbe wote wa Baraza kwa ushirikiano wao wanaotoa katika kutekeleza majukumu ya Kamati.

Kwa kuzingatia kifungu cha 78 ya Katiba ya Zanzibar, 1984, imetoa Mamlaka kwa Baraza la Wawakilishi Kutunga Sheria juu ya mambo yote ya yasiyo ya Muungano.

**"*Nguvu za kutunga sheria kwa mambo yote yasiyokuwa ya Muungano katika Zanzibar yatakuwa mikononi mwa Baraza la Wawakilishi*"**

Pamoja na Mamlaka hayo, Baraza la Wawakilishi kwa mujibu wa Kifungu ya 79(6) ya Katiba ya Zanzibar, 1984 limekasimu madaraka yake kwa mtu yeyote au idara yoyote ya Serikali kutunga

Sheria Ndogo ***(subsidiary legislation/delegated legislation)*** ambazo ni:

i. Amri (Orders)

ii. Matamko (Proclamations)

iii. Kanuni za Taasisi (Rules)

iv. Kanuni za Mahakama (Rules of Court)

v. Kanuni za Wizara (Regulations)

vi. Tangazo

vii. Taarifa(Notices)

Na kwa kuzingatia masharti ya ***Sheria nambari 7/1984. kifungu cha 36 na 37,*** Sheria ndogo au Kanuni inakuwa imekamilika kutungwa baada ya kuwekwa saini na aliyekasimiwa Mamlaka hayo pamoja na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Hivyo, Kamati inaimani kuwa kwa kiasi kikubwa ripoti hii itawezesha Waheshimiwa Wajumbe kupata taaluma na hivyo kuweza kutoa ushauri zaidi kuhusu Kanuni na Sheria Ndogo zinazowasilishwa Barazani kupitia Kamati hii. Aidha, Kamati inamatumaini kuwa Serikali itayafanyia kazi Maagizo yaliyomo katika Taarifa hii na maoni yatakayotolewa na Wawakilishi ili kuondoa dosari zilizobainika kutokana na uchambuzi wa Kamati.
Kabla ya kuendelea naomba nitambue mchango mkubwa uliopelekea kufanikisha kazi hii ya Kamati kutoka kwa Wajumbe wa Kamati ambao wamefanya kazi kwa bidii na maarifa pasi na kuchoka. naomba kuainisha majina yao kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1) Mhe. Mihayo Juma Suleiman N'hunga | Mwenyekiti |
| 2) Mhe. Mwantatu Mbarak Khamis | M/Mwenyekiti |
| 3) Mhe. Mwanaasha Khamis Juma | Mjumbe |

| | |
|---|---|
| 4) Mhe. Hassan Hamad Omar | Mjumbe |
| 5) Mhe. Hudhaima Mbarak Tahir | Mjumbe |
| 6) Mhe. Yussuf Hassan Iddi | Mjumbe |
| 7) Mhe. Suleiman Masoud Makame | Mjumbe. |

Aidha, shughuli za Kamati hii zimekuwa zikiratibiwa na Makatibu wawili kutoka Ofisi ya Baraza la Wawakilishi, ambao wametimiza wajibu wao ipasavyo katika kuhakikisha kwamba Kamati inatekeleza majukumu yake. Makatibu hao wamekuwa chachu ya mafanikio ya kamati kwani wamekuwa wakipokea na kuchambua Kanuni zote zinazowasilishwa na kuwashauri wajumbe namna bora ya kuzifanyia kazi Kanuni hizo na kufanikisha ukamilishaji wa ripoti hii. Naomba nao niwataje kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | |
|---|---|
| 1) Ndg. Karima Abdul- Wahab | Katibu |
| 2) Ndg. Noman Thabit Noman | Katibu |

Vilevile, napenda kumtambua Msaidizi wa Mjumbe ambaye ni:

| | |
|---|---|
| 1) Ndg. Azmina Hamad Khamis | Msaidizi wa Mjumbe |

Kwa mujibu wa kifungu cha 124 cha Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi za toleo la 2024. Kwamba Kamati itawasilishwa Ripoti yake ya mwaka katika mwezi wa Februari. Hivyo basi, kwa mujibu wa masharti hayo. Kamati imetayarisha ripoti hii ili kukidhi sharti hiyo la kisheria.

Ripoti hii ya Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo imegawika katika sehemu kuu tatu (3) nazo ni:

Sehemu ya Kwanza ni Utangulizi, Sehemu ya Pili ni Madhumuni; ambayo inajumuisha Uchambuzi wa Kanuni mbalimbali na Mapendekezo. Sehemu ya Tatu inahusu Hitimisho ya Ripoti hii pamoja na Viambatanisho vya Ripoti hii.

Baada ya utangulizi huo naomba sasa nijielekeze katika ripoti ya Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo kwa mwaka 2024/2025 baada

ya shughuli mbali mbali zilizofanywa na Kamati hii katika kipindi hicho.

Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo katika kutekeleza majukumu yake kwa mujibu wa Sheria imeendelea na kazi zake katika mizunguko yake kama ifuatavyo:
Mzunguko wa Kwanza ulikuwa tarehe ***04/03/2024*** hadi ***22/03/2024,*** Mzunguko wa Pili ulikuwa tarehe ***15/07/2024*** hadi ***02/08/2024*** Mzinguko wa Tatu ulikuwa tarehe ***07/10/2024*** hadi ***25/10/2023*** na Mzunguko wa Nne ulikuwa tarehe ***16/12/2024*** hadi ***6/01/2025.***

Aidha Kamati hii ilipitia Sheria Ndogo na Kanuni mbali mbali kutoka katika Taasisi tofauti kwa dhamira ya kuhakikisha kama Kanuni hizo zimekidhi masharti ya kutungwa kwake pamoja na kuziimarisha ili ziweze kukidhi haja ya kuanzishwa kwake.

Kimsingi kazi ya utungaji wa Sheria ni kazi ya msingi ya Baraza la Wawakilishi. Hata hivyo Kifungu 79(6) cha Katiba ya Zanzibar, 1984, kimekasimu madaraka ya utungaji wa Sheria kwa Idara ama Maafisa wa Serikali ambapo Sheria zinazotungwa kwa utaratibu huo huitwa Kanuni ama sheria ndogo.

kwa kuwa kukasimu madaraka lazima kufuatane na usimamizi (Deligation and Supervision) hivyo Kamati yetu ndiyo yenye jukumu la kufanya kazi ya usimamizi kwa wale waliokasimiwa madaraka hayo kwa niaba ya Baraza. Hivyo Kamati hii inapotekeleza majukumu yake inahakikisha kwamba misingi ya utungaji wa sheria inazingatiwa na kufuatwa kikamilifu kwa kila taasisi au afisa Aliyekabidhiwa majukumu hayo.

Miongoni mwa mambo yanayozingatiwa katika kutunga Sheria ndogo ni pamoja na kuhakikisha Sheria inayotungwa haikiuki Misingi ya Katiba na pia mtunzi wa sheria hiyo awe amepewa Mamlaka na haendi kinyume na Sheria Mama.

Kamati yetu katika kutekeleza majukumu yake, nyezo muhimu tunazotumia kama miongozo ya kazi zetu ni kuzingatia Katiba,

Sheria ya Tafsiri ya Sheria, Sheria ya Utumishi Umma pamoja na Sheria ya Makosa ya Jinai.

Kamati hutumia njia ya kukutana na walengwa wa Kanuni (Wadau) zinazofanyiwa uchambuzi ili kufahamu hali halisi iliopo kuhusiana na sheria husika.
Matumizi ya rejea mbali mbali zilizoandikwa na wataalamu wabobezi pia huwa ni nyezo yetu inayotusaidia kufanya mapitio ya uandishi wa Kanuni hasa suala la utaalamu na mbinu za uandishi.

## 2. MADHUMUNI YA RIPOTI

Ripoti hii unakusudia kueleza utendaji kazi wa Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo, ambapo Kamati inatekeleza majukumu yake kwa kuzingatia masharti ya ***Kanuni ya 119 ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2024,*** ambayo imeainisha majukumu ya Kamati katika ***Jadweli la Kwanza la Kanuni*** *hizo*.

Kamati katika kutekeleza majukumu yake, hutumia njia mbali mbali ili kufikia malengo.

Miongoni mwa njia hizo ni:

- Kupitia nyaraka mbali mbali ambazo Kamati ilikusudia kuzifanyia kazi;
- Kufanya mahojiano na maafisa wanaohusika na Kanuni hizo
- Kufanya mahojiano na walengwa au watumiaji (wadau) wa Kanuni hizo; na
- Kufanya ziara katika Taasisi ambazo kanuni au sheria ndogo hizo zinatumika kama kutakuwa na umuhimu wa kufanya hivyo, ili kuweza kubaini mafanikio na changamoto zao katika utekelezaji wa Kanuni hizo.

Kamati iliweza kutekeleza majukumu yake ipasavyo katika kipindi hiki na kuweza kuchambua Kanuni zilizowasilishwa na kutoa ushauri kwa Taasisi zilizotunga kanuni hizo.

Miongoni mwa majukumu yake ni:

a) kufuatilia utekelezaji wa maagizo ya Kamati yaliyotolewa kwenye Repoti ya Kamati ya Mwaka;

b) Kuchambua kanuni na sheria ndogo ili kujiridhisha iwapo zimekidhi matakwa ya masharti ya Katiba, sheria mama na sheria nyengine;

c) kujadili na kutoa maagizo kwa taasisi husika juu ya namna bora ya kutengeza kanuni na sheria ndogo;

d) kulishauri Baraza kubatilisha Kanuni na Sheria Ndogo ambazo zinakiuka masharti ya Katiba, masharti ya Sheria Mama au Sheria nyenginezo za nchi; na

e) kufikiria jambo jengine lolote litakalopelekwa kwake na Spika.

Kanuni za Baraza zimeweka sharti la kuwasilishwa Barazani Kanuni au Sheria ndogo iliyotungwa na mamlaka nyingine nje ya Baraza la Wawakilishi baada ya kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. Aidha, Kanuni zimetoa fursa kwa Kamati kuitisha kanuni yoyote kwa lengo la kuipitia. Baada ya Baraza la Wawakilishi kupokea kanuni hizo, Kamati hufanya uchambuzi wake na baadae kutoa maoni, maagizo na ushauri juu ya kanuni husika.

Kamati katika kutekeleza majukumu yake imefanikiwa kwa kiasi kikubwa kufikia malengo yake waliyoyakusudia kwa kuzipitia kanuni husika na kubaini mafanikio kwa baadhi ya kanuni licha ya kwamba kumejitokeza baadhi ya changamoto kadhaa kwa baadhi ya kanuni hizo.

Jumla ya Kanuni kumi na sita zilizofanyiwa kazi na Kamati ni:

I. KANUNI ZA KUCHUKUWA WANAFUNZI WA VITENDO, 2023

II. KANUNI ZA MAOMBI YA BARUA MAALUM YA UTAMBUZI WA WAFANYAKAZI WA KIGENI WALIO KATIKA NDOA NA MZANZIBAR, 2023.

III. KANUNI ZA KUMALIZA KOSA, 2023.

IV. KANUNI ZA MASUALA YA DIASPORA, 2023.

V. KANUNI ZA UTOAJI VIBALI VYA MAFUNDI WA UMEME, 2023.

VI. KANUNI ZA MAONESHO NA MATAMASHA YA BIASHARA, 2023.

VII. KANUNI ZA MAUZO KWA MKOPO, 2023.

VIII. KANUNI ZA BIDHAA CHAKAVU, 2023.

IX. KANUNI ZA KAMISHENI YA ARDHI (ADA NA TOZO ZA ARDHI), 2024

X. KANUNI ZA JUMLA ZA MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA, 2023.

XI. KANUNI ZA TAASISI YA WAHASIBU, WAKAGUZI NA WASHAURI ELEKEZI WA KODI, 2023.

XII. KANUNI ZA UDHIBITI NA UZUIAJI WA SUMU KUVU KATIKA BIDHAA ZA CHAKULA, 2023.

XIII. KANUNI ZA JUMLA ZA WATU WENYE ULEMAVU, 2023.

XIV. KANUNI ZA UTUMISHI WA UMMA (USIMAMIZI WA UHAMISHO WA WATUMISHI WA UMMA WANAOHAMISHWA KIKAZI NJE YA UTUMISHI WA UMMA, ZANZIBAR, 2023.

XV. KANUNI ZA UENDESHAJI NA USIMAMIZI WA MASOKO NA MAENEO YA BIASHARA KATIKA MAMLAKA YA SERIKALI ZA MITAA, 2023.

XVI. KANUNI ZA USALAMA WA MAZAO YA CHAKULA, 2023.

Kamati baada ya kuzifanyia mapitio kanuni hizo, ilitaka kujiridhisha juu ya hoja zifuatazo:

a) Utaratibu mzima uliotumiwa na wizara au taasisi katika kutunga kanuni husika.

b) Sababu zilizopelekea kutungwa kwa kanuni hizo.

c) Ushirikishwaji wa Wataalamu mbali mbali wa ndani na nje ya taasisi.

d) Ushirikishwaji wa wadau wanaohusika na kanuni hizo.

e) Baadhi ya kanuni, sheria zake ni za muda mrefu Kamati ilitaka kufahamu kwa nini zilichelewa kutungwa.

f) Changamoto zilizojitokeza kabla ya kutungwa kanuni hizo katika utekelezaji wa sheria.

g) Kulikuwa na utaratibu gani uliotumika kabla ya kutungwa kwa Kanuni hizi na ulikuwa na mapungufu gani pamoja na hayo kanuni hizi zitaweza kuondoa kasoro hizo.

Kamati wakati wa uchambuzi wa Kanuni na Sheria Ndogo zilizowekwa Mezani. Mambo yafuatayo huwa yanazingatiwa:

a) Iwapo kanuni au sheria ndogo husika haiinakiuka Katiba ya Zanzibar, 1984;

b) Iwapo kanuni au sheria ndogo husika inavuka mipaka au kwenda kinyume na masharti ya Sheria inayotoa mamlaka ya kutunga Kanuni na Sheria Ndogo hizo au Sheria nyingine yoyote;

c) Iwapo kanuni au sheria ndogo husika imezingatia misingi bora ya uandishi wa Sheria *(drafting principles)*;

d) Iwapo kanuni au sheria ndogo husika inakiuka misingi ya haki za binadamu;

e) Iwapo kanuni na sheria ndogo inatekelezeka kwa urahisi kwa kukidhi hali halisi ya kiuchumi na kijamii; na

f) Makosa ya Uandishi na uchapaji huzingatiwa katika mapitio ya Kanuni.

Kamati katika kutekeleza wa majukumu yake ilibaini mambo kadhaa kama vile Makosa ya Kimuundo, Makosa ya Kiuandishi, Kimaana, Kiuchapaji na Kisarufi.

Kamati ilizingatia kasoro ilizozibaini na kupendekeza marekebisho na hatua za kuchukuliwa. Miongoni mwa kasoro zilizobainika ni:

a) Baadhi ya kanuni zimeandikwa bila ya kuzingatia vifungu wezeshi (enable provision) vya sheria husika.

b) Baadhi ya kanuni zimeonesha kugongana na Kanuni nyengine au sheria nyengine.

c) Baadhi ya kanuni zimeonesha makosa bila ya kuonesha adhabu inayotokana na kosa hilo.

d) Baadhi ya kanuni hazikuonesha uhalisia wa utekelezaji wa amri inayotolewa na Kanuni hiyo.

Kamati kabla ya kufanya uchambuzi wa Kanuni au Sheria ndogo hulazimika kuipitia sheria iliyotoa kanuni hiyo pamoja na Kanuni husika ili kupata uwelewa na kuweza kufanya uchambuzi utakaosaidia kuimarisha kanuni hizo.

Utaratibu wa kupitia kanuni na sheria ndogo, Kamati huangalia kwa kina maeneo yote ya sheria yanayopaswa kutungiwa kanuni na kuangalia kuwa kanuni hizo zimeenda sambamba na matakwa ya sheria na kuakisi hali iliyokusudiwa.

# 3. UCHAMBUZI WA KANUNI

## 3.1 KANUNI YA WAHASIBU NA WASHAURI ELEKEZI ZANZIBAR, 2023

Kamati ilipitia Kanuni hizo pamoja na kukutana na Wadau walioshiriki katika maandalizi na watumiaji wa Kanuni hizo. Kimsingi Kamati imejiridhisha kuwa Kanuni zimezingatia utaratibu wa uandishi wa kisheria katika kutungwa kwake.

Hata hivyo; Kamati ilibaini changamoto chache katika Kanuni hizo kama ifuatavyo:

### 3.1.1 Makosa ya Uandishi

Kamati katika kupitia Kanuni husika, imebaini makosa ya kiuandishi ambayo yakirekebishwa yataimarisha zaidi Kanuni hizo. Kwa kawaida uandishi wa kanuni na sheria una misingi na taratibu zake na zinaposhindwa kufuwatwa kanuni inaweza kusababisha utata au kupoteza maana iliyokusudiwa. Kamati imebaini makosa ya kiuandishi katika kanuni hizo.

Miongoni mwa makosa hayo ni:

- Kanuni ya 3(h) imeweka neno “**na**” badala ya “**au**” hivyo kubadili dhana iliyokusudiwa.
- Kanuni ya 4(2)(d) maneno **“kama ipo”** hayana umuhimu wa kuwepo kwake. Aidha, mabadiliko hayo yafanyike katika kanuni ya 29(2(d).
- Kanuni ya 7(h),8(2)(j) na 9(2)(j) kanuni zote hizo zimeacha maneno muhimu kwa kuzingatia utaratibu wa uandishi ambayo ni **“kwa kuzingatia masharti ya sheria.”** ambayo yalitakiwa kuwa Mwishoni mwa aya hizo.
- Kanuni ya 11(1)(e) kanuni imeacha maneno **“kanuni za maadili”** baina ya neno **“sheria”** na **“kanuni”**
- kanuni ya 22(c) imeacha maneno **“kwa wakati kulingana na sheria”** mwishoni ili kukidhi utaratibu wa uandishi.

- kanuni ya 22(i) yaingizwe maneno **“kwa mujibu wa Sheria”** mwishoni mwa aya hiyo ili kukudhi utaratibu.

### 3.1.2 Makosa ya Kimantiki

Kwa kawaida kanuni au sheria inapoandikwa lazima iwe inakidhi lengo na inaakisi maana ama mantiki iliyokusudiwa na kuweza kufikisha ujumbe kwa walengwa kukosekana kwa msinhi huo kunaweza kupelekea kutokueleweka kwa kanuni husika, Kamati imebaini makosa kadhaa ya kimantiki katika Kanuni hizo na iwapo hayatarekebishwa yanaweza kuzifanya Kanuni hizo kushindwa kufikisha dhana iliyokusudiwa kwa walengwa kwa urahisi zaidi.

Miongoni mwa makosa hayo ni:

- Kanuni ya 3(i) hii imeweka utaratibu ambao kiutaratibu haupo sawa juu ya nani anayeamua aina za wanachama wanaoweza kusajiliwa kwa kuongeza orodha iliyokwisha kuainishwa jee ni Bodi au Mkurugenzi. kwani kanuni hii ilivyoandikwa Mkurugenzi ndiye mwenye Mamlaka ya kuamua wakati katika utaratibu Bodi ndio yenye Mamlaka hayo.

- Kanuni ya 6(2) katika aya ya (a) maneno **“ushahidi unaoonesha”** yametumika yakiwa na maana ya **“ithibati inayoonesha”**. Aidha, aya ya (a)(ii) ya kanuni hiyo neno **“karatasi”** limetimika badala ya **“machapisho”.**

- Kanuni ya 9(5) haiweki wazi kilichokusudiwa kwani kimantiki **“Bodi inaweza kukubali au kukataa kuidhinisha maombi ya usajili ya muombaji”.**

- Kanuni ya 10, haileti dhana iliyokusudiwa hivyo inashauriwa, kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo: **“Mkurugenzi mtendaji ndani ya siku saba za kazi atamsajili muombaji baada ya idhini ya Bodi”.**

- Kanuni ya 11(1)(h) neno **“kampuni”** linatoa muonekano tofauti na dhana nzima ya neno hilo ndani ya kanuni hizi. Hivyo, Kamati inashauri kufanyiwa tafsri wa neno hilo kwa mamtiki ya kanuni hizi.

- Kanuni ya 11(3), masharti ambayo Mkurugenzi Mtendaji anayoweza kuamua yaanishwe ili iweze kukidhi mahitaji.

- Kanuni ya 24(e) haileti mantiki yoyote kuwepo kwake.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 1 ndani ya Ripoti hii, hivyo kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.1.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 3.2 KANUNI ZA JUMLA ZA WATU WENYE ULEMAVU, 2023

Kamati ilipitia Kanuni za jumla za watu wenye ulemavu, 2023. Kwa ujumla Kanuni hizo zimekidhi matakwa na utaratibu wa kutungwa kwake.

Hata hivyo, Katika kupitia Kanuni hizo Kamati ilibaini makosa kadhaa ambayo iwapo yatarekebishwa yatafanya Kanuni hizi ziwe bora na kuleta tija zaidi kwa walengwa.

Kwa kawaida uandishi wa kanuni una taratibu zake na zisipofuatwa zinaweza kuathiri ubora wa kanuni husika.

Miongoni mwa Makosa yaliyobainika ni:

### 3.2.1 Makosa ya Kiuandishi

- Kanuni ya 4(2)(g) maneno **"na tarehe ya mwisho wa matumizi"** yaliopo mwishoni mwa aya inashauriwa yatoke.
- Kanuni ya 4(2)(h), yaingizwe maneno **"kwa mujibu wa sheria na kanuni hizi"** mwishoni mwa aya hiyo.
- Kanuni ya 5(4), kuongenzwa maneno **"na kutoa uamuzi ndani ya siku ishirini na moja"** mwishoni mwa aya hiyo.
- Baadhi ya maneno ya kimsingi yanahitaji kuwa katika tafsiri lakini hayakuwekwa kama vile. neno **"ulemavu mkubwa"** lilitumika katika kanuni 7(3). Hivyo, Kamati inaagiza kufanyiwa tafsiri.
- Kanuni zieleze uwezo wa **Katibu Mtendaji kukasimu baadhi ya majukumu yake kwa Maafisa wa Baraza.**
- **Suala la** kutumika kwa mtindo mmoja wa uandishi kwa Kanuni nzima ni muhimu, jambo ambalo katika Kanuni hii linakosekana, Kanuni zifuatazo zimekiuka sharti hilo la msingi la uandishi, kanuni ya **7,8,11,15, 16, 17, 18,19, 21, 23, 24, 25, 29,30,31,32, 33 na 35.**

### 3.2.2 Makosa ya Kimantiki

Katika kutungwa kwa kanuni hizi maeneo kadhaa yameandikwa kinyume na dhana inayolengwa na hivyo kuibua makosa ya kimantiki miongoni mwa hayo ni:

- Kanuni ya 4(2)(c), neno **"jinsia"** limetumika likimaanisha **"jinsi".**
- Kanuni ya 5(4), yaingizwe maneno "na kutoa uamuzi ndani ya siku ishirini na moja"
- kuwepo kwa kanuni ambayo imeweka afisa atakayeteuliwa bila kuainisha sifa za uteuzi za afisa huyo.
- Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 2 ndani ya Ripoti hii, hivyo kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.2.3 Mapendekezo;

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

### 3.3 KANUNI ZA MAUZO WA MKOPO, 2023

Kamati ilipitia Kanuni hizo kwa kina pamoja na kukutana na wadau mbali mbali wa Kanuni hizi na kubaini kuwa kuna kasoro ndogo ndogo ambazo zinahitaji kurekebishwa kwa lengo la kuziimarisha, miongoni mwa kasoro hizo ni:

#### 3.3.1 Makosa ya Kimantiki.

Kanuni hii imebaini kwamba tokea awali jina lake linakinzana na mantiki iliyolengwa. Pia kamati imebaini makosa mengine ya kimantiki kwa ujumla makossa ya kimantiki katika kanuni hizo ni kama ifuatavyo:

Jina la Kanuni hizi, ili lilete maana iliyokusudiwa, inapaswa kuingizwa maneno **"kwa njia ya"** baina ya neno **"kwa"** na **"Mkopo".** Aidha, marekebisho hayo yatahusika katika Sehemu yatakapojitokeza maneno hayo ndani ya kanuni hizi.

Kanuni ya 3(2) inarekebishwa kwa kuongezwa aya mpya ya "I" na "j" baada ya aya ya "h" ili iweze kukidhi mantiki ya kuwepo kwake na kusomeka kama ifuatavyo:

(i)muda wa malipo; na

(j) mashahidi.

Kanuni 3, haijaeleza ni ipi kazi au jukumu la msingi la Wizara ya Biashara ndani ya Kanuni hizi.

Kanuni ya 6, inatakiwa kuzingatiwa kwa muda wa malipo ya fidia kulingana na uhalisia wa mkataba.

#### 3.3.2 Makosa ya Kiundishi.

Kwa upande wa makosa ya kiuandishi kamati imebaini makosa mashache katika kanuni hizo kama yanavyoonekana hapo chini:

Kanuni ya 5 inamakosa katika maneno ya pembeni, hivyo ni vyema kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo "**utaratibu wa malipo".**

Kanuni ya 7 kufutwa maneno **"njia ya Amani**" na kuwekwa badala yake "**njia ya makubaliano"**.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 3 ndani ya Ripoti hii, hivyo Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.3.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 3.4 KANUNI ZA KAMISHENI YA ARDHI (ADA NA TOZO ZA ARDHI), 2024

Kamati imefanya mapitio ya Kanuni hizo na kimsingi imejiridhisha kuwa Kanuni zimekidhi matakwa ya kisheria katika kutayarishwa kwake. Hata hivyo, katika kuziimarisha Kanuni hizo Kamati imebaini kasoro chache ambazo zinahitaji kurekebishwa kwa lengo la kuimarisha Kanuni hizo.

### 3.4.1 Makosa ya Kiuandishi

Kanuni hizi zimekiuka misingi ya uandishi wa kanuni kasoro kubwa imeanza kujitokeza katika eneo la kifungu wezeshi ambapo kanuni imeainishwa sheria tofauti na sheria iliyokusudiwa, kwa ujumla makosa ya kiuandishi katika kanuni hizo ni kama yanavyoonekana hapo chini.

Jina la Kanuni hizi, kifungu wezeshi kinarekebishwa kwa kufutwa neno **"na"** na kuweka badala yake **"cha".** Aidha, katika kifungu hicho mwaka wa sheria iliyopelekea kutungwa kwa Kanuni hizi uwekwe sawa kwani usahihi ni ***sheria namba 6 ya mwaka 2015*** na sio ***namba 6 ya 2016***.

Kanuni ya 2, katika maneno ya ufafanuzi, neno **"dini"** kamati inashauri neno hilo lifanyiwe maana kwa dhana matumizi ya ardhi kwa shughuli za kidini.

Kanuni ya 4, irekebishwe kwa kufutwa maneno **"zinafutwa"** na badala yake tuweke maneno **"zinaondoshwa"** (**Revoke**) Aidha, marekebisho hayo yatahusu kanuni ya 4(2).

Kanuni imekosa kuweka masharti yanayohusu Makosa na Adhabu kwa Mtu anayekwenda kinyume na masharti ya Kanuni hizi.

Hivyo Kamati inashauri kuzingatiwa kwa suala hilo. Kwani hata katika Sheria Makosa na adhabu yanayohusu masharti ya Kanuni hizi hayakuainishwa.

Kwa kuwa Kanuni hii utekelezaji wake unahusisha sheria tofauti ni vyema ikawekwa kanuni moja inayozungumzia Makosa na adhabu ambayo itaeleza wazi kuwa **mtu yoyote atakaekiuka masharti ya Kanuni hizi atachukuliwa hatua kwa kuzingatia masharti ya sheria husika.**

### 3.4.2 Makosa ya Kimantiki

Kanuni hizo zimeshindwa kuakisi dhana ya jumla ya kuwepo kwa Tozo inayolengwa kutozwa kupitia kanuni hizo na hivyo kupelekea kupoteza mantiki iliyokusudiwa.

Miongoni mwa makosa ya kimantiki yaliojitokeza ni:

Kanuni haijaweka Tozo kwa upatikanaji wa EKA 3, Kamati inataka kufahamu kama utaratibu wake utakuwa ni bure au kwa njia ya malipo.

Katika ***jadweli Rejea la Upimaji wa Ardhi*** gharama za upimaji zitofautishwe baina ya maeneo yenye idadi kubwa, kati na ndogo ya watu, maeneo yenye idadi ndogo inashauriwa gharama za upimaji ziwe nusu ya eneo yenye idadi kubwa ya watu na maeneo yenye idadi ya kati yawe robo tatu ya idadi kubwa (***4000000, 300000 na 200000.)***

Kanuni imeweka gharama sawa za upimaji kwa maeneo yote. (jadweli kipengele cha ii uk.194). hivyo, ni vyema gharama za upimaji zitofautishwe kama zinavyotofautishwa katika Kodi ya ardhi, na ziweze kuwekwa katika makundi matatu **Maeneo ya Miji (Urban)** ambapo huduma zinapatikana kwa kiasi kikubwa **Maeneo yanayoanza Kukua (Semi Urban)** ambapo huduma ndio kwanza zinaanza na **Maeneo ambayo ni ya vijijini ambayo hayana huduma hizo**. Tozo zitofautiane kulingana na mahitaji. Hivyo Tozo iwe 350000 kama ilivyo sasa kwa maeneo ya Miji ambayo yana huduma, 250000 kwa maeneo ambayo huduma ndio kwanza zimeanza na 150,000 kwa maeneo hayana huduma, kufanya hivyo kunaweza kukachochea baadhi ya wawekezaji kwenda katika maeneo yasio na huduma kama motishani.

Kwa ujumla Kamati imeona kuna haja ya kuangaliwa upya jadweli hilo ili baadhi ya Tozo zitofautishwe kulingana mazingira na sehemu husika na kwa kuzingatia umuhimu wa eneo husika.

Utaratibu katika maeneo ya makaburi (mava uwekwe pamoja na kipengele cha U.K(185) cha Utoaji wa Hati na kipengele cha U.K(195) Upimaji wa Ardhi katika maeneo ya kidini kiwekwe kiwango sawa.

Ada na Tozo za Upimaji au Urasimishaji wa Ardhi zote ziwe katika fedha ya Tanzania pale zoezi linapofanywa kwa Watanzania.

Kuna haja ya kuweka Tozo na Ada kwa kuzingatia uhalisia wa hali za kimaisha za wananchi.

Wakati wa upimaji ni vyema kutoa hati ya kudai malipo ya pamoja ambayo itajumuisha gharama zote badala ya utaratibu wa sasa ambapo hati ya malipo huwa zaidi ya moja.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 4 ndani ya Ripoti hii, hivyo Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.4.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 3.5 KANUNI ZA UENDESHAJI WA MASOKO NA MAENEO YA BIASHARA KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA 2023

Kamati imefanya mapitio ya Kanuni hizi, kwa ujumla Kamati imejiridhisha kuwa Kanuni zimetungwa kwa kufuata misingi na taratibu za kisheria. Hata hivyo, Kamati imetoa maoni yake kwa kupendekeza baadhi ya marekebisho kwa lengo la kuiimarisha Kanuni hizo ili ziweze kufikia Malengo. Kanuni za uendeshaji wa masoko na maeneo ya biashara nazo zimebainika na kasoro kama ifuatavyo:

### 3.5.1 Makosa ya Kiuandishi.

Kanuni hizo zimebainika kuwa na kasoro za msingi katika uandishi wa sheria miongoni mwa kasoro hizo ni kuacha tafsri za maneno muhimu yaliyotumika katika kanuni hizo kwa ujumla kamati imeainisha makosa hayo kama ifuatavyo:

Kamati imeona tafsiri ya '**Mkuu wa Soko'**, haijitoshelezi hivyo inaagiza tafsiri iwe:

**"*Mkuu wa Soko maana yake ni Mtumishi wa Mamlaka aliyeteuliwa kusimamia shughuli zote za soko na maeneo ya biashara*".**

au

***"Mkuu wa soko ni maana yake ni Mtumishi wa Mamlaka aliyeteuliwa kwa mujibu wa Kanuni ya 9 ya Kanuni hizi"***

*Aidha; maneno "**eneo la biashara** "nayo yawekewe tafsiri.*

Kanuni ya 37, Kamati imebaini kuwepo kwa mgongano kwani Kanuni zimemtambua Mkuu wa Eneo la Biashara kama ni mtu mwengine. Hivyo Kugongana na Maana ya Mkuu wa Soko.

Kanuni ya 6, ifanyiwe marekebisho ili iweze kukidhi haja kama ifuatavyo:

a) Aya ya (a) ifutwe.

b) Aya ya (b) yaingizwe maneno **"yanayokiuka taratibu za Kanuni hizi"** baina ya neno **"Kamati"** na **"juu".**

c) Aya ya (d) kuongeza maneno **“kwa kuzingatia Masharti ya Sheria”** mwishon mwa aya hii.

Kanuni ya 12(3) **ifutwe aya ya (a).** kwani huyo Afisa Mapato tayari ni muajiriwa halali wa Serikali ambaye kashaajiriwa kwakuzingatia masharti ya Sheria ya utumishi wa umma na kanuni zake. Hivyo ni jambo ambalo halina msingi kuwepo ndani ya kanuni hizi.

Aidha, kamati inashauri katika matumizi ya neno “**Mfanyakaz**i” na “**Mtumishi”** kuangaliwa ni lipi moja wapo wanahitaji kulitumia Kwani kumejitokeza kutokuwa na uwiano wa matumizi ya maneno hayo ambapo ki uandishi si sahihi.

Kanuni ya 65(2), kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo: **“Katibu Mkuu atasikiliza rufaa hiyo na kutoa uamuzi ndani ya siku saba za kazi kuanzia siku iliyopelekwa rufaa hiyo”.** Aidha, Kanuni izingatie wafanyabiashara ya bidhaa zinazoharibika kwa urahisi.

### 3.5.2 Makosa ya Kimantiki.

Kanuni zimekosa kuainisha baadhi ya maneno muhimu na uhusiano wake katika kuleta mantiki ya kanuni hizo miongoni mwa maeneo hayo ni kama ifuatavyo:

Kanuni hazijaeleza nani mwenye uwezo wa kuanzisha na kusimamia **Eneo ya Biashara.**

Kanuni ya 5, haioneshi mantiki ya kilichokusudiwa.

Kanuni ya 36, haijaweka wazi kuhusu dhana ya “**eneo la wazi**” linalozungumziwa ndani ya Kanuni hizi.

Kanuni ya 57(a) na (b), Kamati inashauri ziangaliwe upya aya hizo kwani haziko wazi kiuandishi. Aidha, aya ya “i”, Kamati inataka kufahamu jee kuna Kanuni inayoweka utaratibu wa uvutaji wa sigara hadharani.

Kamati inashauri Kanuni ya 62 iangaliwe upya kwani kwa ilivyoandikwa inaonekana usafi utafanywa mara moja tu kwa siku ilioteuliwa wakati jambo la usafi linapaswa kufanya kila siku.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 5 ndani ya Ripoti hii, hivyo, Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.5.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 3.6 KANUNI ZA KUMALIZA MAKOSA, 2023

Kamati imefanya mapitio ya Kanuni hizo pamoja na kukutana na wadau husika. Kwa ujumla Kamati imejiridhisha kuwa Kanuni zimetungwa kwa kufuata misingi na taratibu za uandishi wa kisheria. Hata hivyo, Kamati imetoa maoni yake na kuagiza baadhi ya marekebisho kwa lengo la kuziimarisha Kanuni hizo ili ziweze kufikia malengo ya kutungwa kwake.

Miongoni mwa changamoto hizo ni:

### 3.6.1 Makosa ya Kimantiki.

Kamati imeshindwa kuona mantiki halisi ya kuwepo kanuni hizi ambazo zinaelekeza kuwa matumizi yake yatakuwa katika mamlaka mbili zenye kutumia sheria tofauti kwa ujumla kamati imeainisha kasoro katika kanuni hizi kama ifuatavyo:

Kanuni ya 2 inayokuhusu Matumizi ya Kanuni, (Application) ambapo imeeleza kwamba itatumika kwa taasisi zote za **"umma" na "binafsi".**

Kimsingi Masharti ya Kanuni hii yanakinzana na masharti ya kifungu cha ***Matumizi cha Sheria nambari 2 ya 2011,*** na ***Kanuni za Utumishi wa Umma za mwaka 2014.*** Kifungu cha pili cha Sheria hiyo kinaeleza kuwa sheria itakuwa Sheria kiongozi katika masuala yote ya usimamizi wa utumishi wa umma hata kama taasisi ina sheria yake wenyewe.

Mfano katika jadweli la kwanza kipengele cha 11 kinazungumzia kuwa ni kosa kwa muajiri kushindwa kutoa taarifa kwa kamishna juu ya ***kumalizika kwa Mkataba wa Ajira wa Mfanyakazi wa kigeni***.

kimsingi kanuni hiyo inapingana na ***kifungu cha 59 cha Sheria namba 2 ya 2011*** pamoja na ***kanuni ya 95 ya kanuni za utumishi za mwaka 2014,*** ambapo zote kwa pamoja zinaelekeza kwamba ***Ajira ya Mtumishi wa Kigeni*** itatolewa kwa mujibu wa maelekezo ya ***Katibu Mkuu Kiongozi***. Aidha, kuanza na kumalizika kwa Mkataba wa Mtumishi wa Kigeni taarifa zake zinategemea maelekezo ya Katibu Mkuu Kiongozi.

Hivyo basi, Kanuni hii ya Kumaliza Makosa inatengeneza utaratibu wa kuwa na Mamlaka mbili zinazoshughulikia jambo moja.

Makosa mengine yaliyoainishwa katika kanuni hizi, hayawezi kujitokeza katika Utumishi wa Umma kwa mfano kosa katika **Jaduweli la kwanza kipengele cha 2,3,5,6** hayawezi kupatikana katika Utumishi wa Umma. ambapo kosa namba 2 na 3 ajira ya Mtoto Mdogo ambapo katika Utumishi wa Umma anayeajiriwa lazima ufikie umri wa utuuzima, katika msingi huo hakuna mtoto atakaeajiriwa katika utumishi wa umma.

Kamati inashauri kufutwa na kuandikwa upya tafsiri ya Neno **"Afisa Kazi**" na kusomeka kama ifuatavyo:

"**Afisa Kazi". "Maana yake ni Afisa Mkuu wa Kazi Pemba, Maafisa wa Mikoa na Wilaya na inajumuisha Kamishna wa Kazi kama ilivyelezwa chini ya masharti ya Sheria"**

### 3.6.2 Makosa ya Kiuandishi.

Mbali ya makosa ya kimantiki yalioainishwa katika kanuni hizo, kamati imebaini makosa ya kiuandishi kama ifuatavyo:

Pia, katika maneno ya ufafanuzi, neno "**Afisa Muhasibu"** Kamati inashauri kufutwa neno **"au"** liliopo baina ya neno **"na"** na **"matumizi".**

Vile vile, katika neno "**Kamishna",** Kamati inashauri kufutwa neno **"sheria"** lianze kwa kuandikwa kwa herufi kubwa na kuweka **"Sheria"**

Sambamba na hayo, Kamati inashauri neno "**Mkaguzi Kazi"** kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo **"maana yake ni mtu yeyote mwenye haki na wajibu kama ilivyoainishwa chini ya masharti ya Sheria"**

Kanuni ya 5 ya kanuni hizi, Kamati inashauri kufutwa maneno ya pembeni na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo; **"Majukumu ya Afisa Kazi na Mkaguzi Kazi katika Kumaliza Makosa"**

Kamati inashauri kuongezwa kwa kanuni 10, ambayo itaweka sharti ya kwamba **"endapo Mtu au Muajiri atashindwa kutekeleza amri ya kumaliza kosa Kamishna anaweza**

**kuchukua hatua za kufungua mashtaka ya jinai dhidi ya Mtu au Muajiri huyo".**

Mbali na hayo, Kamati inataka kufahamu katika kanuni ya 5 na 6(c) ya kanuni hizi, Afisa Uchuguzi ni nani kwani katika tafsiri ya maneno hakufanyiwa tafsiri.

Kamati inataka ufafanuzi wa kanuni ya 7 ya kanuni hizi kwani kiuandishi haileti maana sawa, hivyo kuangaliwa tena kisheria zaidi.

Kwa ujumla Kamati inashauri Kanuni hizi zifanyiwe marekebisho na Mamlaka yake yabakie kwa watumishi wa Sekta Binafsi tu. Aidha, kwa upande wa Watumishi wa UMMA utaratibu wake umekamilika kupitia Sheria Nambari 2/2011 na Kanuni zake.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 6 ndani ya Ripoti hii, hivyo, Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.6.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 3.7 KANUNI ZA MASUALA YA DIASPORA (USAJILI WA DIASPORA), 2023.

Kamati imefanya mapitio ya Kanuni za masuala ya Diaspora Pamoja na kukutana na Wadau husika. Kimsingi Kamati imejiridhisha kuwa Kanuni zimetungwa kwa kufuata misingi na taratibu za uandishi wa kisheria. Hata hivyo, Kamati imebaini changamoto chache katika Kanuni hizo. Hivyo basi, Kamati imetoa maoni yake kwa kupendekeza baadhi ya marekebisho kwa lengo la kuiimarisha zaidi.

### 3.7.1 Makosa ya Kiuandishi.

Miongoni kwa makosa ya kiuandishi yamejitokeza katika Kanuni hizi, ambayo Kamati inaagiza kuweka vyema kama yafuatayo:
Kanuni ya 2 ya kanuni hizi, kuongezwe tafsiri ya neno **"Mtoto wa Kuasili"** baada ya neno **"Mtoto wa Kulea"** na kusomeka kama ifuatavyo:
**"*maana yake ni mtoto aliyefuata utaratibu wa kisheria kutolewa kwenye usimamizi wa wazazi wake wa asili ambao wana asili ya Zanzibar na kuwa chini ya usimamizi wa Diaspora kwa amri ya mahakama*."**
Vile vile, neno "**Ofisi"** katika neno hilo kuongeza maneno **"kama ilivyoanzishwa kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 4 cha Sheria."** Mwishoni mwa tafsiri hiyo.

Pia, neno **"waliobadilisha utambulisho wao"** maneno haya yameeandikwa kwa uwingi tafsiri yake **(Plural).** Hivyo Kamati inashauri iandikwe vyema kwa kufuata utaratibu wa uandishi mzuri wa kisheria **(Singular)** kama ifuatavyo: **"aliyebadilisha utambulisho wake: maana yake ni mtu wenye asili ya Zanzibar ambaye alibadilisha utambulisho wake wa asili baada ya kuondoka Zanzibar".**
Aidha, neno **"Mtegemezi"** kufutwa na kuandikwa upya ili kuwa katika uandishi mzuri wa kisheria ambapo mtumiaji wa kanuni hizi utamuondoshea shaka. Hivyo itasomeka kama ifuatavyo: **"maana yake ni mtoto wa kuzaa, kulea au wa kuasili wa Diaspora mwenye asili ya Zanzibar.**

Kanuni ya **3(4)** Kamati inashauri kufutwa neno **"mtu"** na kuwekwa badala yake neno **"Diaspora"** kwani kanuni hii inakusudia kuwaondoa katika hatia wana diaspora tu ambao wametoa taarifa zisizo sahihi wakati wa kuomba kusajiliwa.

Kanuni ya 4(d) kuingizwa maneno **"kwa mujibu wa Sheria"** mwishoni mwa aya hiyo ili kuondoa utata kisheria.

Kanuni ya 8(f) kamati inashauri kuongezwa maneno **"kwa kuzingatia masharti ya Sheria**.

Kanuni ya 9(a) kamati inashauri kufutwa neno **"tu"** mwishoni mwa aya hiyo.

Kanuni ya 11(a) kamati inashauri kufutwa neno **"kwa"** liliopo baina ya neno **"kupotelewa"** na **"kitambulisho"** na kuweka badala yake neno **"na"**.

### 3.7.2 Makosa ya Kimantiki.

Kamati katika kuimarisha kanuni hizo imeainisha makosa ya kimantiki kama ifuatavyo:

Kanuni ya **4(c)** Kamati inashauri aya hiyo iangaliwe tena na ni busara kuzingatiwa makosa makubwa ambayo yanahesabika kama ni uhalifu wa kimataifa (***Serious Organize Crime)*** au ***(White Collor Crime).*** kama vile ***makosa ya Dawa za Kulevya, Utakatishaji wa Fedha Haramu na Usafirishaji wa Binadamu.*** Kufanya hivyo kunaweza kufikia manatiki ya Kanuni hizi.

*Aidha, hoja ya kuzingatia miezi sita ya kifungo ni suala zaidi la taratibu za kiutumishi.*

Kanuni ya 10 kamati inashauri maneno **"cha awali"** yatoke kwani yapo mazingira ambayo mtu anaweza kupoteza kitambulisho ambacho si **cha awali** na utaratibu wake haujaelezwa

Aidha, neno **"chake"** lifutwe na kuwekwa badala yake neno **"husika".**

Kamati inashauri kuangaliwa upya kanuni ya 15 kwani suala la ulinzi wa taarifa binafsi ni muhimu sana na lisipochukuliwa kwa tahadhari linaweza kuathiri maisha ya mtu binafsi hivyo adhabu ya

shilighi milioni tano ni ndogo kwa kosa la kutumia taarifa binafsi za mtu.

Aidha, Kamati inashauri adhabu katika kanuni ya 15 ifuate masharti ya adhabu yaliyopo katika kanuni ya 16,17 na 18.

Kanuni ya 19(2) kuongeza maneno **"na kutoa maamuzi kuhusu rufaa hiyo"** mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 7 ndani ya Ripoti hii, hivyo Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.7.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo. Aidha, Kamati inatambua makubaliano ya Mapendekezo ya Kikao cha Majadiliano baina ya Afisi ya Rais – Ikulu, Idara ya Uhamiaji (Zanzibar) na Afisi ya Matukio ya Kijamii kilichofanyika tarehe 18/7/2024. Pamoja na hayo kamati inatarajia kuona utekelezaji wake katika kikao cha kupokea Tarifa za utekelezaji wa Ripoti.

## 3.8 KANUNI YA BIDHAA CHAKAVU, 2023

Kwa ujumla, Kamati inapongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa hali ya juu kutunga Kanuni ya Bidhaa Chakavu**,** 2023,

Kamati imepata mud awa kupitia Kanuni hizi kwa kina pamoja na kukutana na Wadau mbali mbali wa Kanuni hizi. Aidha. Hivyo baada ya Mapitio hayo Kamati imebaini changamoto zifuatazo:

### 3.8.1 Makosa ya Kiuandishi

Kamati katika kimarisha kanuni hizo imeainisha makosa ya kiuandishi ili yaweze kuzingatiwa na kurekebishwa. Miongoni mwa makosa ya kiuandishi ambayo kamati imeshauri, imeagiza pamoja na:

- Kamati inaagiza kifungu cha Sheria kinachotoa uwezo wa kutungwa kwa kanuni hizo, kiandikwa vizuri kwa kuainisha kikamilifu kifungu hicho.
- Katika maneno ya ufafanuzi, neno **"usafirishaji"** linarekebishwa kwa kuingiza neno **"chakavu"** baina ya neno **"bidhaa**" na **"kutoka**"
- Kanuni ya 3(d), kufutwa neno **"au"** na kuweka badala yake neno **"na"** mwishoni mwa aya hiyo. Aidha, Kamati inaagiza kuangalia tena Aya ya (d) imejirejea mara mbili hivyo aya ya (d) moja kuwa (e).
- Kanuni ya 10(d), kuongezwa neno **"chakavu**" mwishoni mwa aya hiyo.
- Kanuni ya 12(1)(b), kufutwa neno "**mkurugnezi"** na kuweka badala yake neno **"mkurugenzi"**.

### 3.8.2 Makosa ya Kimantiki

Aidha, kamati imeainishwa makosa ya kimantika katika kanuni hizo.

Miongoni mwa makosa ya kimantiki ambayo kamati iliyabaini na kushauri pamoja na kuagiza taasisi husika kuyafanyia kazi ni yafuatayo:

Kanuni ya 4(3), haikuainisha sababu zinazopelekea Katibu kukataa maombi ya leseni Kamati inashauri **kuwekwa wazi sababu hizo ndani ya kanuni hizi**.

Kanuni ya 6, Kamati inashauri kuwekwa wazi ndani ya Kanuni hizi sababu za **kukubali au kukataa kuishwa kwa lesini.**

Kanuni ya 7(1), Kamati inashauri kuagaliwa suala la kufutwa kwa lesini lisianze mwanzo lije baada ya **kupewa onyo kwanza** na **endapo akirejea tena kosa hilo ndipo apewe adhabu ya kusitisha leseni iyo**.

Aidha, katika Kanuni ya 7(2), Kamati inashauri kuwekwa utaratibu mzuri wa kusikilizwa mmiliki wa leseni.

Kanuni ya 11, Kamati inashauri **kuainishwa sababu za kukataa maombi ya kibali hicho Katibu Mkuu ndani ya kanuni hizi**.

Kanuni ya 12, Kamati inashauri kuhusu Kamati ya Ukaguzi wa Bidhaa Chakavu, kuangaliwa suala la Muda wa Kamati hiyo uwe miaka 2 au 3

Katika Aya ya (a) Kamati inashauri kama ifuatavyo:

a. Katika (ii)Kufutwa kwa neno **"bidha"** liliopo baina ya neno **"na"** na **"chakuvu"** na kuweka badala yake **"bidhaa"**.

**b.** kuongezwe kwa (iii) na kusomeka kama ifuatavyo: **"kulinda Miundombinu ya Serikali".**

Katika Aya ya (d), Kamati inashauri badala ya Kamati itakagua pawe na Mjumbe ambaye atapewa jukumu la kutoa taarifa kwa Kamati baada ya kukagua.

Kanuni ya 13 (ii) Katika Aya ya (e) na (f) neno **"bidha"** lisomeke **"bidhaa"** na kila lilipojitokeza katika Kanuni hizi.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 8 ndani ya Ripoti hii, hivyo Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.8.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 3.9 KANUNI ZA JUMLA ZA MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR, 2023.

Kamati baada ya kupitia Kanuni hii kwa kina pamoja na kukutana na Wadau, ilibaini kasoro kadhaa miongoni mwa kasoro hizo ni:

### 3.9.1 Makosa ya Kiuandishi.

Miongoni mwa makosa ya kiuandishi ambayo Kamati imeshauri, imeagiza ni pamoja na:

- Baadhi ya Maneno yanahitaji kuwekewa tafsiri, Mfano neno **"Mgeni"** liwekewe Tafsiri**.**
- Baadhi ya Kanuni hazileti tafsiri sahihi hivyo zinahitaji kufanyiwa marekebisho kama:
    - Kanuni ya 3(2)(b) inarekebishwa kwa kuingiza neno **"mchangiaji"** baina ya neno **"mwanachama"** na **"waliopo"**.
    - Kanuni ya 3(2)(c) inarekebishwa kwa kuingiza neno maneno **"mchangiaji"** baina ya neno **"mwanachama"**

na **"uhusiano"**.

- **Aidha,** Kamati inashauri utumiaji wa maneno **"Mwanachama Mchangiaji" na "Mwanachama"** iangaliwe vyema ndani ya kanuni hizi, kwani maneno haya yasipoangaliwa vyema yanaweza kupoteza maana halisi iliyokusudiwa katika baadhi ya kanuni hizi.
- Kanuni ya 5 inarekebishwa katika maneno ya pembeni na kusomeka kama ifuatavyo "**usajili wa mtoto wa kuzaa, kulea au kuasili".**
- Kanuni ya 5(3) inarekebishwa kwa kuingiza maneno **"mchangiaji"** baina ya neno **"mwanachama"** na **"atamsajili"**
- Kanuni ya 5(4) inarekebishwa kwa kuongeza maneno **"na kitambulika kisheria".**

- Kanuni ya 12(c) inarekebishwa kwa kufutwa neno **“na”** na kuweka badala yake neno **“au”** mwishoni mwa aya hiyo.
- Kanuni ya 10(c) inarekebishwa kwa kufutwa neno **“na”** na kuweka badala yake **“au”** mwishoni mwa aya hiyo.
- Kanuni ya 12(a) inarekebishwa kwa kuingiza maneno **“au muajiri”** baina ya neno **“ndugu”** na **“wa”.**
- Kanuni ya 18(d) inarekebishwa kwa kufutwa neno “na” na kuweka badala yake neno “au Kanuni ya 21(4), inarekebishwa kwa kufutwa kwa neno **“upataji”** na kuwekwa badala yake neno **“upatikanaji”**. Aidha, Kamati inataka ufafanuzi wa kanuni hii kwani imebaini mfuko umepewa Mamlaka makubwa.
- Kanuni ya 22(1), kufutwa neno **“itatolea”** na kuweka badala yake neno **“itatolewa”.**
- Kanuni ya 24(2), kuingizwa maneno **“au taasisi”** baina ya neno **“mwanachama”** na **“baada”.** Aidha, marekebisho hayo yafanyike katika mstari wa tatu wa kanuni hiyo.
- Kanuni ya 25(2), kufutwa kwa neno **“zilizotajwa”** liliopo baina ya neno **“dharura” na “chini.**

### 3.9.2 Makosa ya Kimantiki

Kamati katika kupitia kanuni hizo imeshindwa kuona mantiki ya kuwepo kwa baadhi ya kanuni kutokana na kasoro za kimantiki zilizojitokeza.

Miongoni mwa makosa ya kimantiki ambayo Kamati iliyabaini na kushauri pamoja na kuagiza taasisi husika kuyafanyia kazi ni yafuatayo:

Kanuni ya 3(2)(d) Kamati inahitaji ufafanuzi kwani kiuandishi inaonekana kuwa na utata.

Kanuni ya 8, Kamati inahitaji ufafanuzi zaidi. Aidha, Kuhusu kutambuliwa kwa vitambulisho vya kielektroniki.

Kanuni ya 24(4), Kamati inataka kufahamu kuhusu muda wa kumuarifu muombaji kwa nini haukuainishwa. Aidha, utaratibu wa rufaa upoje endapo hakuridhika na maamuzi hayo.

Kanuni ya 33(a), Kamati inataka kufahamu rufaa hiyo inaenda kwa nani kiutaratibu iainishwe ndani ya kanuni hii.

Kanuni ya 49(1)(d), Kamati inashauri katika kanuni hiyo mamlaka yabaki kwa Bodi au Mkurugenzi Mkuu na sio kwa Kamati ya Bodi inayohusiana na ukaguzi kwani kwa kawaida Kamati ya Bodi inakuwa haina mamlaka ya Mwisho ya Maamuzi.

Kanuni ya 16, Kamati inashauri kufutwa na na kuandikwa upya kwa Kanuni hiyo na kuiepusha na kuipeleka katika Ujinai na badala yake masuala haya yamalizwe katika utaratibu wa kiutawala zaidi**.**

Kanuni ya 20(3), Kamati inataka kufahamu na ufafanuzi wa kutosha kuhusu kubadilisha utaratibu wa ngazi za vituo vya utoaji wa huduma za afya kwamba Wiziri au Mfuko ndio unaoweza kubadilisha.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 9 ndani ya Ripoti hii, hivyo Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.9.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 3.10 KANUNI YA KUCHUA WANAFUNZI WA VITENDO 2023

Kwa ujumla, Kamati inapongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa hali ya juu kutunga Kanuni za kuchukuwa wanafunzi wa vitendo.

Kamati imepata muda wa kupitia Kanuni hizo kwa kina pamoja na kukutana na Wadau mbali mbali wa Kanuni hizo. Kwa ujumla Kanuni zimefuata taratibu za uandishi na zimekidhi haja kwa kiasi kikubwa. Hivyo baada ya Mapitio hayo Kamati imebaini changamoto zifuatazo:

### 3.10.1 Makosa ya Kiuandishi

Miongoni mwa sharti la msingi katika uandishi wa kanuni ili iweze kutumika ni kutangazwa katika Gazeti Rasmi na ni lazima maelezo ya kuwa kanuni itaanza kutumika wakati gani yaanishwe wazi. Hivyo, miongoni mwa makosa ya kiuandishi ambayo kamati imeshauri, imeagiza pamoja na:

Kanuni ya 1, Kamati inashauri kuongezwe maneno **"na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali"** kwani ni matakwa ya uandishi wa kanuni kwa mujibu wa sheria ya tafsiri ya sheria kuwa Kanuni haiwezi kutumika mpaka itapotangazwa katika Gazeti la Serikali.

Kanuni ya 4(2), katika Aya(a), Kamati inashauri neno **"au"** kufutwa na badala yake liandikwe katika Aya ya **"b"** ya kanuni ndogo hiyo. Ili iendane na utaratibu wa uandishi.

Kanuni ya 5(2), Kamati inashauri kuwekwa maneno **"maombi hayo"** mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo.

Kanuni ya 5(3), Kamati inashauri kufutwa neno **"wake"** mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo.

Kanuni ya 6(1), Kamati inashauri kufutwa kwa namba **"5"** iliopo baina ya **"ya"** na **"ya"** na kuwekwa badala yake **5(1).**

Kanuni ya 10, Kamati inashauri kufutwa neno **"madktari"** na kuweka badala yake neno **"madaktari".**

### 3.10.2 Makosa ya Kimantiki

Baadhi ya maeneo katika kanuni hizo hayaleti taswira ya kilichokusudiwa hivyo kupelekea kushindwa kupatikana kwa

mantiki. Miongoni mwa makosa ya kimantiki ambayo Kamati iliyabaini na kushauri pamoja na kuagiza taasisi husika kuyafanyia kazi ni yafuatayo:

- Kamati inataka ufafanuzi wa kanuni ya 4(3) ili kujiridhisha kwani haieleweki imekusudiwa nini kuwepo kwake.
- Kanuni ya 7(1), Kamati inataka kufahamu ni wanafunzi wa aina gani ambao wanaotakiwa kulipwa posho.
- Kanuni ya 8(a), Kamati inataka ufafanuzi wa aya hiyo nini wamekusudia.

Kwa ujumla maeneo hayo yote hayajakidhi mantiki ya kuwepo kwake kwani walengwa hawapati uwelewa wa kutosha juu ya maana iliyokusudiwa.

Aidha, Kamati inataka kuelewa kwa jee ilipotungwa kanuni hizi zilizingatia Sheria ya ZSSF kuhusu fao la kumia kazini namna gani imetambua haki za wanafunzi wa vitendo wanapopata matatizo wakiwa kazini.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 10 ndani ya Ripoti hii, hivyo Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.10.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 3.11 KANUNI ZA MAOMBI YA BARUA MAALIMU YA UTAMBUZI KWA WAFANYAKAZI 2023

Kamati ilipitia Kanuni hizi kwa undani pamoja na kukutana na Wadau walioshiriki katika matayarisho yake Pamoja na watumiaji wa Kanuni hizo na kubaini changamoto kadhaa licha ya kwamba Kanuni hizi zimezingatia utaratibu wa uandishi wa kisheria. Hivyo Kamati katika kuhakikisha Kanuni hizi zinafikia lengo la kuanzishwa kwake inapendekeza marekebisho katika maeneo mbali mbali kama ifuatavyo:

### 3.11.1 Makosa ya Kiuandishi:

Kanuni yoyote ni lazima itangazwe katika Gazeti Rasmi kabla ya kuanza kutumika kwake. Kamati imebaini makosa ya kiuandishi katika kanuni hizo kama ifuatavyo:

Kanuni ya 1, irekebishwe kwa kuongezwa maneno **“na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali”** kwani ni matakwa ya uandishi wa kanuni kwa mujibu wa sheria ya tafsiri ya sheria, Kanuni haiwezi kutumika hadi ikitangazwa katika Gazeti Rasmi

Kanuni ya 3 ya tafsiri ya maneno inarekebishwa katika maneno yafuatayo:

**“kamishna”** neno **“sheria”** linafutwa na kuandikwe “**Sheria”** kwani katika uandishi ukiandika sheria **“S”** inamaanisha ni sheria mahsusi wa jambo unaloliongelea.

**“ndoa”** Kamati inataka kufahamu maana ya neno hili limefanyiwa tafsiri ipi kwa mujibu wa sheria kwani ni vyema kuweka tafsiri kwa mujibu wa sheria au tafsiri inayotambuliwa na sheria.

**“Zanzibari”** Kamati inashauri kuandikwa neno hilo **“Mzanzibari”** kwani aliyefanyiwa tafsiri ni Mzanzibar.

Kanuni 4(2) Kamati inashauri kufuta neno **“chini”** liliopo baina neno **“maombi”** na **“ya”.**

Kanuni 4(2)(c) Kamati inashauri kufuta maneno **“cha sasa”** na kuweka badala yake neno **“halali”**.

Kanuni ya 4(2)(l), Kamati inashauri kuongezwa kwa maneno **“kwa mujibu wa sheria”** mwishoni mwa aya hiyo.

Kanuni ya 5(2), Kamati inashauri kuongezwa maneno **"kwa kuzingatia masharti ya sheria"**

Kanuni ya 6(2) inarekebishwa kwa kufuta neno **"huko"** na kuweka badala yake maneno **"maombi hayo"**

Kanuni ya 6(3), Kamati inashauri kufutwa kwa maneno **"wa kamishna"** yaliopo mwishoni mwa kanuni hiyo.

### 3.11.2 Makosa ya Kimantiki

Kamati imebaini kuwa baadhi ya dhana katika kanuni hizo hazipo wazi na hivyo kushindwa kuakisi mantiki.

Miongoni mwa makosa ya kimantiki ambayo Kamati iliyabaini na kushauri pamoja na kuagiza taasisi husika kuyafanyia kazi ni yafuatayo:

- Kanuni ya 4(2)(b) Kamati inataka kufahamu sababu za kuwekwa kwa kiambatanisho hicho kwani ilivyo haionekani mantiki ya kuwepo kwake.
- Kanuni ya 4(2)(d) Kamati inataka kufahamu jee ikiwa hana nakala ya hati ya kusafiria nini kifanyike.
- Kanuni ya 4(2)(h) Kamati inataka kufahamu nini hasa kinatakiwa wakati muombaji ni raia.
- Kanuni ya 4(2)(g) Kamati inataka kufahamu sababu za kuwekwa kwa kiambatanisho hicho. Aidha, ni lipi lengo na nini wajibu wa polisi, kwani ilivyoandikwa haiwezi kuleta mantiki halisi ya kuwepo kwake.
- Kanuni ya 4(2)(i) Kamati inataka kufahamu sababu za kuwekwa kwa kiambatanisho hicho. Aidha, Mkataba wa kazi wa nani ni wa muombaji au anayemuombea. Hivi ilivyo haioneshi mkataba huo unamuhusu nani, hivyo kanuni inapoteza mantiki yake.
- Kanuni ya 8 Kamati inataka kufahamu kwa wale ambao wanataka kuongeza Mkataba wao utaratibu wake utakuwaje? Kwani kanuni haikuweka wazi.

- Kanuni ya 11, Kamati inataka kufahamu jee suala la eda imezingatiwaje.pia kuhusu siku 14 Kamati inataka kufahamu ni zipi wamekusudia.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 11 ndani ya Ripoti hii, hivyo Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.11.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 3.12 KANUNI ZA UTOAJI VIBALI KWA MAFUNDI WA UMEME,2023

Kamati ilipitia Kanuni hizi pamoja na kukutana na Wadau wanaohusiana na Kanuni hizo. Kimsingi Kanuni zimefuata taratibu za kutungwa kwake. Hata hivyo; Kamati imebaini changamoto ambazo zikirekebishwa zitaimarisha zaidi Kanunu hizo. Hivyo Kamati katika kuhakikisha Kanuni hizi zinafikia lengo la kuanzishwa kwake inapendekeza marekebisho katika maeneo mbali mbali kama ifuatavyo:

### 3.12.1 Makosa ya Kiuandishi

Kamati imebaini kuwa katika Kanuni hizi kuna baadhi ya makosa ya kiuandishi. Miongoni mwa hayo ni kutokueleweka kwa baadhi ya ufafanuzi wa maneno. Hivyo Kamati imetoa ushauri na maagizo ya marekebisho kama ifuatavyo:

- Kamati inapendekeza kanuni ya 3(5) kufuta neno "ya" liliopo baina ya neno **"faini"** na **"isiyopungua"**

- Kanuni ya 6(2) ifutwe maneno **"kwa kuongezea katika vigezo vilivyoainishwa katika Kanuni hizi na kwa matakwa ya Mamlaka"** na kuweka badala yake maneno **"kwa kuzingatia masharti yaliwekwa katika kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii Mamlaka inaweza kumfanyia majaribio ya maandishi, mdomo na vitendo muombaji**.

Uandishi uliopo sasa haukidhi matakwa ya uandishi.

Kamati inashauri Kanuni ya 7(1) kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

"**Mamlaka itahakiki uhalali wa taarifa zilizomo na kuamua kukubali ombi la kutoa kibali au kukataa la muombaji"**

Kamati inashauri maneno ya pembeni ya kanuni ya 10, kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

**"Muda wa uhalali wa kibali"**

### 3.12.2 Makosa ya Kimantiki

Miongoni mwa makosa ya kimantiki ambayo Kamati iliyabaini na kushauri pamoja na kuagiza taasisi husika kuyafanyia kazi ni yafuatayo:

- Kanuni 2, Kamati ilitaka kupatiwa ufafanuzi zaidi ya maneno yafuatayo:
    - **"Kazi Maalum"**,
    - **"Mafundi Umeme" na**
    - **"Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)".**

Maneno hayo yametumika katika ufafanuzi lakini ufafanuzi wake haujitoshelezi.

- Kanuni ya 3(3), Kamati inataka kufahamu na kupata ufafanuzi kuhusu maneno **"miezi isiyozidi mitatu"** inakusudia nini?

Jee iwapo itazidi miezi mitatu nini kinafanyika? Ni lazima Kanuni iweke wazi utaratibu unaotakiwa kufanyika.

Kamati inashauri kuangaliwa umuhimu wa uwepo wa **"kibali cha muda mfupi"** katika kanuni ya 12, kwa wale wanaotaka kufanya maombi ya kazi za muda tu ambao watakuwepo nchini. Kufanya hivyo ndio kunaweza kuleta mantiki ya Kanuni hiyo.

Kamati inashauri kuandikwa kanuni mpya ambayo itaweka katazo la ***Mpewa kibali kutoruhusiwa kuhaulisha kibali hicho kwa mtu mwengine yeyote***."

Kamati inaagiza Kanuni ya 4(2)(e) kuangaliwa tena kwani haipo wazi. Aidha, inaitaka Mamlaka kuhakikisha viambatanisho vyote vinavyohitajika kuambatanishwa na fomu A ya Jadweli la kwanza la kanuni hizi, viainishwe ili kuondoa utata wa kisheria kwa muombaji na kuepusha Mamlaka kutumia madaraka nje ya mipaka ya Sheria

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 12 ndani ya Ripoti hii, hivyo Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.12.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 3.13 KANUNI ZA MAONESHO NA MATAMASHA YA BIASHARA YA 2023

Kamati ilipitia Kanuni hizo pamoja na kukutana na Wadau husika. Licha ya Kanuni hizi kukidhi baadhi ya Masharti ya uandishi wa Kanuni, Hata hivyo; Kamati imebaini changamoto kadhaa ambazo zisiporekebishwa zitaleta athari kubwa katika matumizi yake.

*Kanuni za Maonesho na Matamasha ya Biashara ya 2023*, imeanzishwa chini ya kifungu 54(1) cha Sheria nambari 14 ya mwaka 2013

Kimsingi, Kamati inajukumu la kuhakikisha Kanuni zimekidhi matakwa ya uandishi wa Kanuni kwa kuzingatia masharti ya sheria.

Utaratibu wa kutunga Kanuni upo kisheria jambo la kuzingatia Kanuni yoyote inayotungwa itokane na Sheria na anayetunga awe amepewa Mamlaka hayo na Sheria husika, ni lazima kiwepo kifungu wezeshi (enable provision) kinachotoa maelekezo ya kutungwa kwa Kanuni na kutoa Mamlaka kwa mtunzi wa Kanuni. Bila ya kutimizwa kwa masharti hayo Kanuni inayotungwa huwa ni **batili tokea awali (void ab initio).**

Miongoni mwa makosa ya kimantiki ambayo Kamati iliyabaini na kushauri pamoja na kuagiza taasisi husika kuyafanyia kazi ni yafuatayo:

Kamati imebaini kwamba kanuni hii imeende nje ya mipaka yake hivyo inataka kufahamu uwezo walioutumia Wizara ya Biashara kutunga kanuni hizi, kwani:

Kwa mujibu wa Sheria Kuanzisha Ofisi ya Mufti namba 4 ya mwaka 2021, chini ya kifungu cha 4(j), kifungu cha 37 na kifungu cha 52(2) (b).

Mamlaka ya Waziri anayesimamia Ofisi ya Mufti ndiye mwenye dhamana ya kutunga ***kanuni inayohusiana na uratibu wa sherehe za kidini*** ambapo Kanuni ya Maonesho na Matamasha imeingilia uwezo huo, ambapo kiutaratibu Kanuni hiyo haiwezi kuandaa utaratibu unaotekelezwa kupitia sheria nyengine.

Aidha, Kanuni hizi pia, zimeenda kuingilia Sheria ya Baraza la Sanaa nambari 7 ya mwaka 2015 chini ya uwezo waliopewa Waziri katika kifungu cha 29(b) ya ***Kuratibu matamasha ya kiutamaduni na kushajihisha kutunzwa kwa utamaduni katika ngazi za Wilaya.***

Kwa mantiki hiyo, ***Kanuni za Maonesho na Matamasha ya Biashara ya 2023,*** haiwezi kuwa juu ya sheria inayohusiana na utamaduni,

Kamati katika kulipatia ufumbuzi suala hilo ilikutana na Waziri anayesimamia masuala ya Utamaduni, Waziri anayesimamia Ofisi ya Mufti na Waziri mwenye dhamana ya Masuala ya Biashara kwa lengo la kujadili mustakbali wa Kanuni hizo.

Hivyo, Kamati inahitaji ufafanuzi wa ya hoja hizo zilizojitokeza kutoka kwa wizara husika ili kuweza kuendelea na hatua nyingine za maamuzi pamoja kufanya majumuisho na kuishauri Wizara husika.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 12 ndani ya Ripoti hii, hivyo Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.13.1 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 3.14 KANUNI ZA USALAMA WA MAZAO YA CHAKULA

Kamati ilipitia Kanuni hizi pamoja na kukutana na Wadau wanaohusiana na Kanuni hizo. Kimsingi Kanuni zimefuata taratibu za kutungwa kwake. Hata hivyo; Kamati imebaini changamoto ambazo zikirekebishwa zitaimarisha zaidi Kanunu hizo. Hivyo Kamati katika kuhakikisha Kanuni hizi zinafikia lengo la kuanzishwa kwake inapendekeza marekebisho katika maeneo mbali mbali kama ifuatavyo:

### 3.14.1 Makosa ya Kiuandishi.

Miongoni mwa makosa ya kiuandishi ambayo Kamati iliyabaini na kushauri pamoja na kuagiza taasisi husika kuyafanyia kazi ni yafuatayo:

Kanuni ya 6(g) Kamati inashauri kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo: **"Kukagua mazao yenye viashiria vya sumu kuvu au yaliyoripotiwa kuwa na sumu kabla ya kutumika au kuchakatwa".**

Aidha, Kamati inashauri kuongezwa kwa aya mbili mpya ambayo itaweka utaratibu wa ukaguzi wa wafanyabiashara.

**"(h) kuanzisha kitengo mahsusi cha ukaguzi wa viuatilifu vya wafanya biashara; na**

**(i) kuweka utaratibu wa fidia za gharama za uzalishaji kwa mkulima atakaetoa taarifa za sumu kuvu katika mazao yake na ikathibitika."**

### 3.14.2 Makosa ya Kimantiki

Miongoni mwa makosa ya kimantiki ambayo Kamati iliyabaini na kushauri pamoja na kuagiza taasisi husika kuyafanyia kazi ni yafuatayo:

Kanuni ya 2 (1), Waziri aongeze zao la mpunga katika jadweli la kwanza ninaloonesha orodha ya mazao chini ya kanuni hizi ili kuweza kulijumuisha katika mazao hayo.

Kamati inaagiza katika kanuni ya 4(1)(b) kuongezwa maneno “**na udhibiti wa viatilifu hivyo baada ya matumizi.”** Mwishoni mwa aya hiyo.

Kanuni ya13, Kamati inaagiza kanuni kuandikwa upya kwa kuweka wajibu wa wizara kuainisha vigezo na masharti ya vyombo vya usafiri vitakavyotumika kusafirishia mazao.

Kanuni ya 7(2), Kamati inashauri kuingizwa maneno **“au bwana shamba wa eneo husika”** mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo.

Kanuni ya 7(3), Kamati inashauri kuingizwa maneno **“au bwana shamba wa eneo”** baina ya neno **“Wilaya”** na **“husika”.**

Kanuni ya 7(4), Kamati inashauri kuingizwa maneno **“au bwana shamba wa eneo husika”** baina ya neno **“Wilaya”** na **“ametenda”.**

Kamati inashauri kuongezwa maneno **“na Afisa huyo anaweza kutoa ruhusa ya uvunaji kwa kuzingatia soko na mahitaji ya zao husika.**

Kanuni ya 7(4) kamati inaagiza kuongezwa maneno “na akipatikana na hatia atachukuliwa hatua kwa kuzingatia masharti ya kanuni hizi.

Aidha, marekebisho hayo yatafanyika kila yatakapojitokeza maneno hayo ndani ya kanuni hizi kama 8(3),9(3), 10(3), 11(3) na 12(3) na nyenginezo.

Kanuni ya 15(1)(a) Kamati inashauri kuongeza maneno **“Afisa Kilimo Wilaya au Bwana Shamba wa Shehia husika**” mwishoni mwa aya hiyo.

Kamati inashauri aya ya 15(1)(b) ifutwe. Aidha, kuwekwe utaratibu wa kuteketeza mazao hayo yenye sumu kuvu. Vile vile, Kamati inataka kufahamu utaratibu wa mazao yanayotoka nje ya Zanzibar ukoje.

Vile vile, Kamati inashauri kuwekwe kanuni itakayoweza kudhibiti sumu kuvu pamoja na kuwekwa utaratibu mzuri wa kudhibiti sumu kuvu kwa mazao yanayotoka nje ya Zanzibar.

Kanuni ya 15(3), Kamati inashauri maneno Mamlaka husika yawekwe wazi ni ipi imekusudiwa ndani ya Kanuni hii. Aidha,

marekebisho hayo yafanyike kila yanapojitikeza maneno hayo ndani ya Kanuni hizi.

Kanuni ya 17, Kamati inashauri kufutwa maneno **"Mkurugenzi"** na kuweka badala yake **"Afisa Kilimo wa Wilaya"** sababu kila wilaya ina afisa wa kilimo. Aidha, tumeiwekea ujinai isipotekelezwa hivyo tunatakiwa kuwekea urahisi wa kutekezwa (compliance).

Pia, idadi ya wakulima ni kubwa kuhudumiwa na mkurugenzi mmoja nchi nzima, visiwa vyetu ni Unguja na Pemba kumtoa mtu sehemu moja kwa kufata huduma hiyo wizarani ni usumbufu na inaweza kupelekea kutotiiwa kwa sheria hiyo.

Kuongezwa kanuni ndogo ya 2 mpya na kusomeka kama ifuatavyo: **"Maafisa wa Kilimo wa Wilaya atatoa taarifa za usajili wa wakulima kwa kwa Mkurugenzi".**

Aidha, kuongezwa kanuni ndogo ya 3 ambayo itaonesha **Vigezo Vya Usajili wa Mkulima.**

Pamoja na marekebisho hayo ndani ya Kanuni hiyo, Kamati inaagiza Kanuni ya ndogo ya 2 kuwa ya 4.

Kanuni ya 18, Kamati inashauri kurekebishwa kwa kufutwa neno **"Mkurugenzi"** na kuwekwa badala yake **"Afisa wa Kilimo wa Wilaya**" mwanzoni mwa kanuni hiyo.

Aidha, Kanuni ya 18(2) neno **"Mkurugenzi"** hilo pia litafutwa na kuwekwa **"Afisa wa Kilimo wa Wilaya**"

Aidha, kuwekwe kanuni ndogo ya 3 mpya ambayo itaonesha mazingira ambayo yanaelezea; **"iwapo Mkulima anayeomba kusajiliwa hajatimiza vigezo vya kusajiliwa, Afisa wa Kilimo wa Wilaya atamuelekeza kwenda kukamilisha vigezo hiyo."**

Kamati inaagiza Kanuni ya 18(2) kuwa 18(4) na inafutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo;

**"endapo Afisa wa Kilimo wa Wilaya atakataa ombi la usajili la muombaji baada ya kushindwa kukamilisha vigezo vya usajili wa mkulima, atamuarifu muombaji kwa maandishi na sababu za kukataa huko."**

Kamati inashauri kuongezwa Kanuni 18(5) mpya na kusomeka kama ifuatavyo; **“endapo ombi la kusajiliwa limekataliwa muombaji anaweza kukata rufaa kwa mkurugenzi ndani ya siku kumi na nne za kazi na mkurugenzi anatakiwa kuitolea uamuzi rufaa hiyo ndani ya siku kumi nan ne za kazi tokea kupokea rufaa hiyo.”**

Kamati inashauri kuongezwa Kanuni 18(6) mpya na kusomeka kama ifuatavyo; **Rufaa kutoka kwa mkurugenzi itawasilishwa kwa waziri ndani ya siku kumi na nne za kazi na Waziri atatakiwa kuitolea uamuzi rufaa hiyo.**

kanuni ya 20(1) inarekebishwa kwa kufutwa maneno “litatunzwa na mkurugenzi” na kuweka badala yake maneno **“litakuwa chini ya Usimamizi wa Mkurugenzi”**

Kanuni ya 20(2)(c) inarekebishwa kwa kuingiza maneno **“au Kitambulisho cha Mtanzania (NIDA)”**

Kamati inashauri Kanuni ya 20(2)(g) inarekebishwa kwa kuongeza maneno **“kwa mujibu wa Sheria na kanuni hizi”** mwishoni mwa aya hiyo.

Kanuni ya 21, Kamati inashauri kurekebishwa kwa kufutwa maneno **“iliyotolewa atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani”** na kuwekwa badala yake maneno **“haikuainishwa na akipatikana na hatia”** baina ya neno **“maalum”** na **“atalipa”.**

Kanuni ya 7, Kamati inaagiza kuwekwa utaratibu wa maombi ya ruhusa na muda wa kujibiwa maombi hayo uweke wazi, ili kuondosha au kupunguza urasimu kwa wakulima na wafanya biashara.

Kamati unaagiza kuangaliwa kwa upande wa mfanyabiashara. Aidha, Adhabu na Utaratibu wake uwekwe vyema ndani ya kanuni hizi. Rejea; kanuni ya 15 na Sehemu ya Pili maneno ya Kichwa cha Habari zimetambua wafanyabiashara na wakulima.

Kamati inaagiza kuangaliwa vyema kanuni ya kudhibiti na uingizaji wa sumu kuvu katika bidhaa za chakula 2023 inayotokana na Sheria nambari 2 ya mwaka 2006, kwamba hazigongani na kanuni hizi ili kuweza kudhibiti muingiliano wa kanuni hizo.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 13 ndani ya Ripoti hii, hivyo Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.14.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 3.15 Kanuni za Utumishi Wa Umma (Usimamizi Wa Uhamisho Kwa Watumishi Wa Umma Wanaohamishwa Kikazi Nje Ya Utumishi Wa Zanzibar), 2024

Kamati imepitia kanuni hizo pamoja na kukutana na Wadau husika ili kuangalia ushiriki katika maandalizi wa kanuni hizo,baada ya kupitia kanuni hizo kamati imebaini kuwa licha ya kwamba taratibu ya utungwaji wa kanuni zimefuwatwa lakini kanuni hizo zimekuwa na changamoto kadhaa ambazo zisiporekebishwa dhamira ya kuwepo kwa kanuni hizo haitafikiwa. Miongoni wa changamoto hizo ni:

### 3.15.1 Makosa ya Uandishi

Katika uandishi wa kanuni taratibu na misingi ya uandishi ni lazima yazingatiwe ili kanuni ziweze kufikia malengo na kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa walengwa. Miongoni mwa makosa ya kiuandishi ni matumizi yasio sahihi ya dhana zinazotumika katika kuandika sheria pamoja na kutoyatumia maneno kwa muhtadha unaokusudiwa.

Baadhi ya Makosa ya Uandishi katika kanuni hizo na marekebisho yanayopendekezwa ni kama yafuatayo:

- kanuni ya 2(a) kuingizwa maneno mapya **"muungano wa"** baina ya maneno **"ya"** na **"Tanzania"**.

Aidha, katika kanuni hiyo Kamati pia inatendekeza kuangaliwa upya neno "**inajumuisha"** katika kanuni hii kuwepo kwake ni utata kisheria.

- Kamati inapendekeza kanuni ya 3 kufanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:

a) Katika ufanunuzi wa neno **“Mamlaka ya usimamizi wa Nidhamu”** kufutwa kwa maneno **“ya utumishi wa Umma**” baina ya neno **“Sheria”** na **“au”.**

b) Katika ufanunuzi wa neno “**Nje ya utumishi wa umma”** lisomeke “**Uhamisho nje ya utumishi wa umma”**.

- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 8 kufutwa kwa neno **“kuathiri”** liliyopo baina ya maneno “**Bila ya”** na “**masharti”** na kuwekwa badala yake neno **“kujali”.**

- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 10(2) kufutwa kwa neno **“mtumishi”** liliyopo baina maneno **“mtumishi”** na **“wa umma”.**

- Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni ya 13 kama ifuatavyo:

  a) Kanuni ya 13(4) inafanyiwa marekebisho kwa:

     i. kufutwa neno **“yeyote**” liliyopo baina maneno **“umma**” na **“ambaye”.** na

     ii. kufutwa maneno **“ambayo hatozingatiwa katika utumishi wake”** yaliyopo baada ya maneno **“sekta binafsi”.**

  b) Kanuni ya 13(5) inafanyiwa marekebisho kwa kufutwa kanuni ndogo hiyo.

- Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni ya 16(3) kama ifuatavyo:

  a) Kwa kufutwa maneno **“nyongeza ya mshahara au**” yaliyopo baina ya maneno **“kumpatia**” na **“bonasi”.**

  b) Kwa kufutwa neno **“ummt”** na kuwekwa badala yake neno **“umma”.**

- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 21 kufutwa kwa maneno **“sekta binafsi”** yaliyopo baina maneno **“sekta binafsi”** na **“itakuwa”.**

- Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni ya 25(4) kama ifuatavyo:

  a) Kwa kufutwa maneno **“mma**” yaliyopo baina ya maneno **“utumishi wa**” na **“atakuwa”** na kuwekwa badala yake neno **“umma”.**

  b) Kwa kufutwa neno **“mma” liliyopo mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo** na kuwekwa badala yake neno **“umma”.**

### 3.15.2 Makosa ya Kimantiki

- Kamati inapendekeza neno **“Masuala ya Kiutumishi**” linalopatikana katika kanuni ya 3 ya Kanuni hizo lifanyiwe tafsiri upya kwani masuala ya kiutumishi hayaishii tu kama yalivyoainishwa katika kanuni bali yapo mengine yanayohitajika kuwepo katika neno hilo la ufanunuzi.

- Kamati inaitaka Wizara kuangalia vizuri mantiki iliyokusudiwa katika kanuni ya 13(4) na 23 kwa mtumishi wa umma atakaekataa kwa makusudi matakwa ya Serikali, je masharti ya kanuni hiyo hayapingani na Kanuni ya 63 ya utumishi ya mwaka 2014.

Je, likizo bila ya malipo huwa inatolewa na muajiri au mtumishi lazima aiombe. Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 63 ya mwaka 2014 likizo bila ya malipo inamuda maalum?

Je, likizo bila ya malipo inayotolewa na kanuni hizi ina muda gani?

- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 19 maneno **"pande zote mbili"** zikafafanuliwe vizuri ili zijulikanwe kwa urahisi.

- Kamati inapendekeza maneno **"Mkataba Maalum"** na **"Mkataba Mama"** yaliotumika katika Kanuni hizi kufanyiwa tafsiri.

- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 3 katika neno **"Mkuu wa Taasisi"** kufutwa kwa maneno "**Katibu Mkuu"** ambapo neno hilo "**Katibu Mkuu"** inashauriwa liwe na tafsiri yake inayojitegemea.

- Kamati inashauri katika matumizi ya maneno bila ya kuathiri na bila ya kujali yaangaliwe upya kwani kutumika kwake bila ya umakini kutapelekea kutoteza dhana zima ya kanuni ilivyokusudiwa ndani ya kanuni hizi.

Aidha, Maagizo mengine yanajionesha katika Kiambatanisho Nambari 14 ndani ya Ripoti hii, hivyo Kamati inasisitiza kuzingatiwa maagizo hayo ipasavyo.

### 3.15.3 Mapendekezo

Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni hizo kama ilivyoainishwa hapo juu ili ziweze kufikia malengo.

## 4. HITIMISHO

Kamati inaimani kuwa Serikali itayafanyia kazi mapendekezo yaliyomo katika Ripoti hii na maoni yatakayotolewa na Wajumbe wa Baraza ili kuondoa dosari zilizobainika kutokana na uchambuzi wa Kamati katika Kanuni husika.

Kamati inashauri Wizara, Mamkala, Mashirika na Taasisi zote kwa ujumla ambazo zimekasimiwa madaraka hayo na Baraza la Wawakilishi kuhakikisha kwamba Kanuni zao walizokwisha kuzitunga au wanazotarajia kuzitunga waziwasilisha katika Kamati hii ya Kanuni na Sheria Ndogo ambayo kwa niaba ya Baraza la Wawakilishi ina jukumu la msingi kuhakikisha Kanuni zote pamoja na Sheria Ndogo hazijatoka nje ya mipaka na zimefuata utaratibu kikamilifu ili dhana ya kukasimu madaraka iweze kufikiwa kwani endapo kutakuwa na dhana ya kukasimu madaraka kunaenda sambamba na usimamizi wa madaraka hayo.

Pamoja na maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla Taasisi zenye Kanuni hapo juu, Kamati inatoa maoni, ushauri na mapendekezo ya jumla kama ifuatavyo:

a) Ushirikishwaji wa Wadau na wahusika wengine ufanyike katika hatua za uandishi wa Kanuni. Katika dhana hii Kamati inashauri taasisi ambazo zimepewa mamlaka ya kutunga kanuni kwa lengo la utekelezaji mzuri wa sheria, kuhakikisha kwamba utaratibu wa ushirikishwaji wa wadau katika utungwaji wa kanuni husika. Kwani Kamati, ilibaini changamoto hiyo katika baadhi ya Kanuni wakati wa kuchukua maoni ya Wadau, kwamba walikosa fursa ya kushiriki katika utungwaji wa Kanuni hizo;

b) Kamati inaishauri Wizara kusimamia kikamilifu utekelezaji wa Kanuni hizo, kwani kuwa na Sheria na kanuni zake nzuri ni jambo moja na utekelezaji wake ni jambo jingine tofauti. Hivyo Wizara zisimamie utekelezaji huo;

c) Kutolewe Elimu kwa Umma, Watendaji na Watumiaji kabla au wakati Kanuni zinatungwa ili wafahamu utekelezaji wa Kanuni. Kwani mantiki ya Kamati kushauri juu ya kupatiwa elimu wa Kanuni husika watendaji na watumiaji ikijumuisha jamii kwa ujumla, juu ya uwepo wa Kanuni hizo, ni kuweza kurahisisha utekelezaji wake;

d) Kamati inaishauri Wizara ambazo zilishauriwa kukutana, ili kutatua changamoto za muingiliano wa majukumu ndani ya kanuni ya Maonesho ya Biashara, yatekelezwe kwa umakini zaidi, ili kuepusha mgongano wa kisheria na Kanuni zake pamoja na muingiliano wa majukumu katika Sheria nyengine. Kwani Mamlaka wakati wa kutunga Kanuni hutakiwa kuzingatia kwamba kanuni au sheria ndogo haikiuki misingi ya Katiba na pia haendi kinyume au kugongana na Sheria Mama au Sheria nyengine.

e) Kamati inashauri kwa ujumla wakati wa kutungwa kanuni mambo muhimu ya kuzingatiwa ni pamoja na kuhakikisha kwamba kanuni inafuata taratibu za uandishi wa kanuni ikijumuisha **"Jina fupi na kuanza kutumika"** ikifuatana na kutiwa saini na na aliyekasimiwa mamlaka hayo pamoja na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali. ***Kama inavyoshurutishwa katika kifungu cha 36 na 37 cha Sheria ya Ufafanuzi Nam.7 ya 1984;***

f) Serikali iweke Muongozo wa Utunzi (draft manual) ili kuwe na muelekeo unaofanana wa Kanuni (consistency); na

g) Marekebisho ya Sheria ya Tafsiri ya Sheria yafanyike haraka ili kuwa na sheria inayokwenda na mahitaji ya hivi sasa.

Mwisho; Napenda kutumia fursa hii kutoa shukrani zangu za dhati kwako binafsi na Baraza lako tukufu kwa kuendelea kutuamini na kutupa nafasi sisi wajumbe wako kuendelea kuhudumu katika Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo na kutuwezesha leo kuwasilishwa Ripoti yetu katika Baraza lako tukufu. Ni matumaini yetu kuwa, utaratibu huu utakuwa endelevu na umuhimu wa Kamati hii na Kamati nyenginezo katika maendeleo ya nchi yetu. Aidha tunaishukuru Afisi ya Katibu wa Baraza na wasaidizi wake kwa kuhakikisha kuwa uwepo wa Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo ni muhimu sana kwa kuwa kwa kiasi kikubwa Kanuni na Sheria ndogo ndizo zinagusa maisha ya kila siku ya wananchi wengi.

Kipekee kabisa naomba nimshukuru Mhe. Haroun Ali Suleiman, Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi wa Umma kwa mashirikiano yake kupitia maafisa wao kufanikisha majukumu yetu kwa urahisi. Aidha, niwashukuru Mawaziri, Makatibu Wakuu na Wakuu wa Sekta, mbali mbali kwa kufika mbele ya Kamati na kujibu hoja zilizoibuliwa na Wajumbe wa Kamati.

# 5. VIAMBATANISHO

## 5.1 KIAMBATANISHO NAMBARI 1
## Kanuni ya Wahasibu na Washauri Elekezi Zanzibar 2023

Kamati ilipitia Kanuni hizi kwa undani pamoja na kukutana na Wadau walioshiriki kutunga na watumiaji wa Kanuni hizo na kubaini changamoto kadhaa licha ya kwamba Kanuni hizi zimezingatia utaratibu wa uandishi wa kisheria. Kwa kuwa Kamati hii inajukumu la kuhakikisha changamoto hizo zinarekebishwa ili kuwa kanuni iliyo bora.

Kamati inashauri katika kanuni ya 2 katika ufafanuzi wa maneno kuingizwa tafsiri ya neno **"kampuni"** kwa mantiki ya kanuni hizo nini inakusudiwa kwani maana halisi ya kampuni inatambua mtu mmoja anaweza kuwa na kampuni lakini ndani ya kanuni hizi kama ya 8 na 29(4)(g) unashurutisha kuwepo hati ya ubia.

Kanuni ya 3(h) inarekebishwa kwa kufuta **"na"** na kuweka **"au"**

Aidha, Kamati inataka kufahamu kanuni ya 3(h) imekusudiwa nini.

Kanuni ya 3(i) kamati inataka kufahamu ni nani anayeamua aina za wanachama wanaoweza kusajiliwa kwa kuongeza orodha iliyokwisha kuainishwa jee ni Bodi au Mkurugenzi kwani kanuni hii ilivyoandikwa Mkurugenzi ndiye mwenye Mamlaka ya kuamua wakati katika utaratibu bodi ndio yenye Mamlaka.

Kanuni ya 4(2)(d) kamati inashauri maneno **"kama ipo"** yatoke kwani hakuna muajiri asije kuwa na anuani. Aidha, marekebisho hayo yafanyike katika kanuni ya 29(2)(d) ya kanuni hizi.

kanuni ya 6(2) inarekebishwa kama ifuatavyo:

Aya ya (a) kufuta neno **"ushahidi"** na kuweka badala yake maneno **"ithibati inayoonesha"** mwanzoni aya hiyo.

Aya ya (a)(ii) kufuta neno **"karatasi"** na kuweka badala yake neno **"machapisho".**

Kanuni ya 7(h), kamati inashauri kuingizwa maneno **"kwa kuzingatia masharti ya sheria." Mwishoni mwa aya hiyo.**

Kanuni ya 8(2)(f) kamati inataka kufahamu jee ubia ni lazima.

Kanuni ya 8(2)(j), Kamati inashauri kuingizwa maneno **"kwa kuzingatia masharti ya sheria."** Mwishoni mwa aya hiyo.

Kanini ya 9(2)(f), Kamati inashauri kuingizwa maneno **"kwa kuzingatia masharti ya sheria."** Mwishoni mwa aya hiyo.

Kamati inashauri Kanuni ya 9(5) kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo; **"Bodi inaweza kukubali au kukataa kuidhinisha maombi ya usajili ya muombaji".**

Kamati inashauri kuongeza aya mpya ya9(6) na kusomeka kama ifuatavyo: **"endapo Bodi itakataa kuidhinisha maombi ya usajili mkurugenzi mtendaji atamtaarifu muombaji kwa maandishi na kuainisha sababu za kukataa huko ndani ya kipindi cha siku saba za kazi".**

Kanuni ya 10, Kamati inashauri kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo: **"Mkurugenzi mtendaji ndani ya siku saba za kazi atamsajili muombaji baada ya idhini ya Bodi"**

Kanani ya 11**(1)(b)** kamati inashauri iangaliwe upya kwani uzoefu wa wenzetu upo tofauti kwa upande wao wanazuia matumizi ya leseni badala ya kuifuta.

Kamati inashauri Kanuni ya 11(1)(e) kwa kuingiza maneno **"kanuni za maadili"** baina ya neno **"sheria"** na **"kanuni"**

Kanuni ya 11(3), Kamati inashauri masharti ambayo Mkurugenzi Mtendaji anayoweza kuamua yaanishwe.

Kamati inashauri Kanuni ya 22(c) kuingiza maneno **"kwa wakati kulingana na sheria"** mwishoni mwa aya hiyo.

Kamati inashauri Kanuni ya 22(h) kufuta maneno **“na yeye”** yaliopo mwishoni mwa aya hiyo.

Kamati inashauri Kanuni ya 22(i) kuingiza maneno **“kwa mujibu wa Sheria”** mwishoni mwa aya hiyo.

Kamati inashauri Kanuni ya 23(d) kuingiza neno **“kupitia”** mwazoni mwa aya hiyo.

Kanuni ya 24(a) kuingiza maneno **“kwa mujibu wa sheria”** mwishoni mwa aya hiyo.

Kanuni ya 24(d) kuingiza neno **“kushauri”** mwanzoni mwa aya hiyo.

Kanuni ya 24(e) kamati inashauri kuondolewa kwa aya hiyo.

Kanuni ya 24(o) kuingiza maneno **“kwa mujibu wa sheria”** mwishoni mwa aya hiyo.

**Naomba kuwasilisha**

**……………………………………….**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

## 5.2 KIAMBATANISHO NAMBARI 2

## KANUNI ZA JUMLA ZA WATU WENYE ULEMAVU, 2023

Kamati ilipitia kanuni hizi kwa undani pamoja na kukutana na Wadau walioshiriki kutunga na watumiaji wa kanuni hizo na kubaini changamoto kadhaa licha ya kwamba kanuni hizi zimezingatia utaratibu wa uandishi wa kisheria.

Kwa kuwa Kamati hii inajukumu la kuhakikisha changamoto hizo zinarekebishwa ili kuwa na kanuni zilizobora. Hivyo basi, Kamati imependekeza yafuatayo kwa ujumla:

- Kanuni ya 4(2)(c), Kamati inashauri kufutwa kwa neno **"jinsia"** na kuwekwa badala yake neno **"jinsi".**
- Kamati inapendekeza kuwepo na kanuni mpya ya "**6(2)"** ambayo itahusu taarifa kupewa mtu aliefutiwa usajili.
- Kamati inaagiza katika kanuni ya 8(2)(a) kuongezwa kwa maneno "**na mamlaka"** baada ya neno **"kilichothibitishwa".**
- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 8(2)(d) kuongezwa kwa maneno "**kwa mujibu wa sheria"** baada ya neno **"Mtendaji".**
- Kamati inapendekeza neno **"ulemavu mkubwa"** lilitumika katika kanuni 7(3) lifanyiwe tafsiri kwenye kanuni ya ufafanuzi.
- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 13(3) kuengezwa kwa maneno **"ya kupokea barua**" baina ya maneno "**tarehe"** na **"ya".**
- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 14(1)(a) kuingizwa kwa maneno "**ushiriki katika**" mwanzoni mwa aya hiyo.

- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 17 kuengeza aya mpya ya **"d"** itakayohusu **"muongozo wa burudani na michezo kwa watu wenye ulemavu"** na aya zilizobakia kufuata mtiririko wake wa kialfabeti.
- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 8(2)(d) kuengezwa kwa maneno "**kwa mujibu wa sheria"** baada ya neno **"Baraza".**
- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 35 kufutwa kwa neno **"itateuwa"** liliyopo baina ya neno "**wizara"** na neno "**itateuwa"** na kuwekwa badala yake maneno **"itashirikiana na Katibu Mtendaji katika kuteuwa"**.

**MAONI YA MAREKEBISHO YA KISARUFI**

1. Kamati inapendekeza katika kanuni ya 3(2)(c) kufutwa kwa maneno **"Sheha na Shehia"** na kuwekwa badala yake **"sheha wa shehia".**
2. Kamati inapendekeza katika kanuni ya 3(2)(e) kufutwa kwa maneno **"Daktari au Afisa"** na kuwekwa badala yake **"daktari au afisa".**
3. Kamati inapendekeza katika kanuni ya 8(2)(b) kufutwa kwa maneno **"Katiba ya Jumuiya"** na kuwekwa badala yake **"katiba ya jumuiya".**
4. Kamati inapendekeza katika kanuni ya 8(2)(c) kufanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:

   **a.** Kwa kufutwa kwa maneno **"Sheha na Shehia"** na kuwekwa badala yake **"sheha wa shehia".**

   **b.** Kwa kufutwa kwa neno **"Jumuiya"** na kuwekwa badala yake **"jumuiya".**

5. Kamati inapendekeza katika kanuni ya 11 kufutwa kwa maneno **“Mpango wa Utekelezaji”** na kuwekwa badala yake **“mpango wa utekelezaji”.**

6. Kamati inapendekeza katika kanuni ya 13(1), (2) na (3) kufutwa kwaneno **“Jumuiya”** na kuwekwa badala yake **“jumuiya”.**

Kamati inapendekeza kutumika kwa mtindo mmoja wa uandishi wa maneno ya **“watu wenye ulemavu**” au “**Watu Wenye Ulemavu”** katika Kanuni hizi, maeneo ya kuyazingatia ni kwenye kanuni ya **7,8,11,15, 16, 17, 18,19, 21, 23, 24, 25, 29,30,31,32, 33 na 35.**

7. Kamati inapendekeza katika kanuni ya 17(3) kufutwa kwa maneno **“Kitaifa, Kikanda na Kimataifa chini ya Mikataba”** na kuwekwa badala yake **“kitaifa, kikanda na kimataifa chini ya mikataba”.**

8. Kamati inapendekeza katika **Jadweli la kwanza** katika ukurusa wa 17 kufutwa kwa maneno **“Maoni ya Katibu Mtendaji”** na kuwekwa badala yake **“Maamuzi ya Katibu Mtendaji”.**

**MAONI YA JUMLA YA KAMATI**

1. Kamati inapendekeza kuwepo kwa kanuni mpya itakayoainisha sifa za mtu atakaeteuliwa kuwa Afisa Mratibu.

2. Kamati inapendekeza kuwepo na sehemu itakayotambua taratibu za utambuzi wa Vyama vya Ushirika vya Watu wenye Ulemavu.

3. Kamati inapendekeza kuwepo na sehemu itakayotambua taratibu za utambuzi wa Vyama vya Michezo vya Watu Wenye Ulemavu.

4. Kamati inashauri Kanuni itambue uwepo wa watu wenye ulemavu wa muda mfupi ili nao wasije kukosa fursa kama wanazopata watu wenye ulemavu wa aina nyengine.

**Naomba kuwasilisha**

……………………………………….

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

## 5.3 KIAMBATANISHO NAMBARI 3

## KANUNI ZA MAUZO WA MKOPO

Kwanza kabisa Kamati inapongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa hali ya juu kutunga Kanuni za Mauzo wa Mkopo 2023, ambazo zinaendana na hali halisi iliyo sasa.

Aidha, Kamati itafanya Majumuisho aina mbili ya kwanza ya uwasilishwaji wa nyaraka ambapo michango mengi ya Wajumbe wa Kamati yamo ndani ya waraka huu.

Aidha, mbali na waraka huu Wajumbe wa Kamati watakuwa na fursa ya kuchangia zaidi Kanuni hizi wakati tunapowasilisha waraka huu endapo watakapohitaji kufanya hivyo na yatakuwa miongoni mwa mapendekezo au ushauri wa Kamati.

Kamati baada ya kupitia Kanuni hii kwa kina pamoja na kukutana na Wadau mbali mbali wa Kanuni hizi. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kupitia Kanuni hiyo na kubaini mambo yafuatayo:

Katika jina la Kanuni, Kamati inashauri kuingiza maneno **"kwa njia ya"** baina ya neno **"kwa"** na **"Mkopo"** katika eneo jina la kanuni. Aidha, marekebisho haya yatafanyika kila yatakapojitokeza maneno hayo katika Kanuni hizi.

Katika jina la kanuni, kamati inashauri kurekebishwa kwa kuandikwa upya jina hilo na kusomeka kama ifuatavyo ***"KANUNI ZA MAUZO KWA NJIA YA MKOPO, 2023.*** Aidha, marekebisho hayo yatafanyika kila yatakapojitoke maneno kama hayo ndani ya Kanuni hizi.

Kanuni ya 1, inarekebishwa kwa kufutwa neno **"zitajilika"** liliopo baina ya neno "**hizi"** na **"kama"** na kuweka badala yake neno **"zitajulikana"**

Katika Sehemu ya Pili, Kichwa cha Habari kinarekebishwa kwa kuongeza maneno **"kwa njia"** baina ya neno **"kwa"** na **"mkopo"**

Kanuni ya 3(1) inarekebishwa kwa kufuta maneno **“na mauzo”** yaliopo baina ya neno **“msambazaji”** na **“kwa”** na kuweka badala yake maneno **“wa mauzo kwa njia ya mkopo”**

Kanuni ya 3(2) inarekebishwa kwa kuingiza maneno **“njia ya”** baina ya neno **“kwa”** na **“mkopo”.**

Kanuni ya 3(2) inarekebishwa kama ifuatavyo:

(a) Aya ya (e) kwa kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka “**utaratibu wa malipo”.**

(b) Aya ya (g) kwa kufutwa neno **“na”** mwishoni kwa aya hiyo.

(c) kuongezwa kwa aya mpya ya “i” na “j” baada ya aya ya “h” na kusomeka kama ifuatavyo:

**(i) muda wa malipo; na**

**(j) mashahidi.**

Katika Kanuni ya 3(3) ya Kanuni hii, Kamati inashauri kuangaliwa upya kwa upana zaidi ili kuhakikisha makubaliano hayo yanathibitishwa na mawakili.

Vilevile, Kamati inashauri **Mamlaka husika** iweke sharti kwa wahusika wa mkataba kutoa taarifa kwamba endapo pande yoyote ya makubaliano anataka kufanya mabadiliko yoyote katika mkataba huo lazima atoe taarifa hiyo ya mabadiliko hayo mfano **jina, hisa au kauza kampuni kwa mtu mwengine wakati wanapofunga mkataba huo.**

Aidha, Kamati inataka kufahamu kwa mujibu wa kanuni 3, hii ni ipi kazi au jukumu la msingi la Wizara ya Biashara.

Kanuni ya 5, inarekabishwa katika maneno ya pembeni kwa kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo **“utaratibu wa malipo”**

Kanuni ya 6, katika Kanuni hii inaelezea endapo upande wowote wa Mkataba umevuja makubaliano hayo upande utakaoumizwa utalipwa fidia. Kamati inataka kufahamu nani atakuwa na uwezo wa kusimamia upatikanaji wa fidia hiyo kwa upande ulioumizwa.

Aidha, Kamati inashauri kuzingatiwa kwa muda wa malipo ya fidia hiyo kulingana na uhalisia wa Mkataba huo.

Kanuni ya 7 inarakabishwa kwa kufutwa maneno **“njia ya Amani**” na kuwekwa badala yake maneno “**njia ya makubaliano”**.

Kanuni ya 8, Kamati inashauri kufutwa kwa maneno “**Mahakama Kuu**” na badala yaka kuwekwa chombo chenye mamlaka ya kisheria kusikiliza shauri hilo.

Kamati inashauri kuzingatiwa utaratibu wa rufaa ndani ya kanuni hizi. kuelezwa

**Naomba kuwasilisha**

**……………………………………….**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

## 5.4 KIAMBATANISHO NAMBARI 4

**KANUNI ZA KAMISHENI YA ARDHI (ADA NA TOZO ZA ARDHI)**

Kwanza kabisa Kamati inapongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa hali ya juu kutunga **Kanuni za Kamisheni ya Ardhi (Ada na Tozo za Ardhi)** ambazo zinaendana na hali halisi iliyo sasa.

Kiutaratibu Kamati hii inajukumu la kuhakikisha kasoro hizo zinarekebishwa ili kuwa na Kanuni iliyobora zaidi na hapo ndipo ule uwepo wa dhana ya kukasimu madaraka inatekelezwa kwa vitendo.

Aidha, Kamati itafanya Majumuisho aina mbili ya kwanza ya uwasilishwaji wa nyaraka ambapo michango mengi ya Wajumbe wa Kamati yamo ndani ya waraka huu.

Aidha, mbali na waraka huu Wajumbe wa Kamati watakuwa na fursa ya kuchangia zaidi Kanuni hizi wakati tunapowasilisha waraka huu endapo watakapohitaji kufanya hivyo na yatakuwa miongoni mwa Mapendekezo au Ushauri wa Kamati.

Kamati baada ya kupitia Kanuni hii kwa kina pamoja na kukutana na Wadau mbali mbali wa Kanuni hizi. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kupitia Kanuni hiyo na kubaini mambo yafuatayo:

Kwanza kabisa Kamati inashauri katika Jina la Kanuni, kifungu wezeshi kinarekebishwa kwa kufuta neno **"na"** na kuweka badala yake **"cha"**

Aidha, Kifungu wezeshi, (enable provision) kilichompa uwezo Waziri kutunga Kanuni hizi Kamati inashauri kuangaliwa upya na kwa umakini zaidi mwaka wa sheria husika kuwekwa vyema kwani mwaka halisi wa sheria hiyo ni sheria namba 6 ya mwaka 2015 na sio namba 6 ya 2016.

Kamati inashauri katika Kanuni ya 2, ufafanuzi wa maneno

Kamati inashauri neno **"dini"** lifutwe na kuwekwa badala yake neno **"maana yake ni matumizi ya ardhi kwa shughuli za kidini"**

Aidha, Kamati inashauri katika eneo la utoaji wa Hati za Shamba kwa taasisi za dini nalo lizingatiwe kwa kuwekwa kima chake.

***Rejea (jadweli umiliki wa haki za matumizi ya ardhi, kipengele cha iii)***

***Rejea Kipengele cha iv kinachozungumzia eka tatu (3)*** hakuna Tozo zilizowekwa, Kamati inataka kufahamu kama utaratibu wake utakuwa ni bure.

Kamati inashauri katika Kanuni ya 4, irekebishwe kwa kufutwa maneno **"zinafutwa"** na badala yake tuweke maneno **"zinaondoshwa".** Kwani kanuni hazifutwi bali zinaondolewa (**Revoke**) Aidha, marekebisho hayo yatahusu kanuni ya 4(2), pia.

Kanuni imekosa kuweka masharti yanayohusu Makosa na Adhabu kwa Mtu anayekwenda kinyume na masharti ya Kanuni hizi.

Hivyo Kamati inashauri kuzingatiwa kwa suala hilo. Kwani hata katika Sheria Makosa na adhabu yanayohusu masharti ya Kanuni hizi hayakuainishwa.

Kamati inashauri neno "Ada" na "Tozo" kufanyiwa tafsiri ya maneno hayo.

Katika ***jadweli Rejea kipengele cha i la Upimaji wa Ardhi*** gharama za upimaji zitofautishwe baina ya maeneo yenye idadi kubwa, kati na ndogo ya watu, maeneo yenye idadi ndogo inashauriwa gharama za upimaji ziwe nusu ya eneo yenye idadi kubwa ya watu na maeneo yenye idadi ya kati yawe robo tatu ya idadi kubwa (***4000000, 300000 na 200000.)***

Kamati inashauri katika jadweli kipengele cha ii uk.194 gharama za upimaji zitofautishwe na ziweze kuwekwa katika makundi matatu **Maeneo ya Miji (Urbau)** ambapo huduma zinapatikana kwa kiasi

kikubwa **Maeneo Yanayoanza Kukua (Semi Urban)** ambapo huduma ndio kwanza zinaanza na **Maeneo ambayo ni ya vijijini ambayo hayana huduma hizo**. Tozo nitofautiane kulingana na mahitaji. Hivyo Tozo iwe 350000 kama ilivyo sasa kwa maeneo ya Miji ambayo yana huduma 250000 kwa maeneo ambayo huduma ndio kwanza zimeanza na 150,000 kwa maeneo hayana huduma, kufanya hivyo kunaweza kukachochea baadhi ya wawekezaji kwenda katika maeneo yasio na huduma. Kama motishani.

Kamati inashauri kwa ujumla kuangaliwa upya jaduweli hilo ili baadhi ya Tozo zitofautishwe kulingana mazingira na sehemu husika na kwa kuzingatia umuhimu wa eneo husika.

Katika maeneo ya makaburi (mava uwekwe pamoja na kipengele cha U.K(185) cha Utoaji wa Hati na kipingele cha U.K(195) Upimaji wa Ardhi katika maeneo ya kidini kiwekwe kiwango sawa.

Ada za Tozo za Upimaji au Urasimishaji wa Ardhi zote ziwe katika fedha ya Tanzania pale zoezi linapofanywa kwa Watanzania.

1. Kuna haja ya kuweka Tozo na Ada kwa kuzingatia uhalisia wa hali za kimaisha za watu wetu ambao wengi ni maskini sana.

2. Kamati inashauri Kamisheni ya Ardhi ifanyekazi ya kutoa huduma kwa jamii na sio Kukusanya Mapato zaidi hasa inapohudumia watu wa ndani kwenye shughuli zisizo za kibiashara. Hii itasaidia wananchi wengi kumudu kurasimisha kuhaulisha Ardhi zao na hivyo kuweza kupunguza migogoro ya ardhi katika jamii.

Aidha, itawawezesha kiuchumi kwa vile ni ardhi iliyorasimishwa tu ndio ambayo mmiliki anaweza kuchukulia mkopo wa benki ili kufanya biashara.

3. Wakati waupimaji Kamati inashauri kutoa hati ya kudai malipo moja ambayo itajumuisha gharama zote badala ya utaratibu wa sasa ambapo hati ya malipo huwa zaidi ya moja.

Kwa kuwa kanuni hii utekelezaji wake unahusisha sheria tofauti ni vyema ikawekwa kanuni moja inayozungumzia Makosa na adhabu ambayo itaeleza wazi kuwa **mtu yoyote atakaekiuka masharti ya kanuni hizi atachukuliwa hatua kwa kuzingatia masharti ya sheria husika.**

**Naomba kuwasilisha**

.............................................

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

## 5.5 KIAMBATANISHO NAMBARI 5

## KANUNI ZA UENDESHAJI WA MASOKO NA MAENEO YA BIASHARA KATIKA MAMLAKA ZA SERIKALI ZA MITAA

Kwanza kabisa Kamati inapongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa hali ya juu kutunga ***Kanuni za Uendeshaji wa Masoko na Maeneo ya Biashara katika Mamlaka za Serikali za Mitaa 2023,*** ambazo zinaendana na hali halisi ya ya Masoko na Maeneo ya Biashara kama yalivyo sasa.

Aidha, Kamati itafanya Majumuisho aina mbili ya kwanza ya uwasilishwaji wa nyaraka ambapo michango mengi ya Wajumbe wa Kamati yamo ndani ya waraka huu.

Aidha, mbali na waraka huu Wajumbe wa Kamati watakuwa na fursa ya kuchangia zaidi Kanuni hizi wakati tunapowasilisha waraka huu endapo watakapohitaji kufanya hivyo na yatakuwa miongoni mwa mapendekezo au ushauri wa Kamati.

1. Kwa kuanza katika Kanuni ya 2, Kamati inashauri kuangaliwa vyema tafsiri ya neno Mkuu wa Soko kwa mujibu wa Kanuni hizi. Aidha, Kamati inashauri tafsiri hiyo inaweza kuwa kama ifuatavyo:

    "*Mkuu wa Soko maana yake ni Mtumishi wa Mamlaka aliyeteuliwa kusimamia shughuli zote za soko na maeneo ya biashara" rejea Kanuni ya 10,11,27***.** au

*"Mkuu wa soko ni maana yake ni Mtumishi wa Mamlaka aliyeteuliwa kwa mujibu wa Kanuni ya 9 ya Kanuni hizi".*

Kamati inashauri hivyo ili kuonekane tofauti baina ya maana ya neno **"Mkuu wa Soko"** na **"Mamlaka ya Uteuzi wa Mkuu wa Soko"** kwani Kanuni ya 12 imezungumza wazi uwezo wa Mkurugenzi wa kumteua Mkuu wa Soko.

2. Kamati imebaini Kanuni ya 37 imemtambua **Mkuu wa Eneo la Biashara** kama ni mtu mwengine. Kamati inataka ufafanuzi wa nadharia hiyo ndani ya Kanuni hizi jee Mkuu wa eneo la biashara ndiye Mkuu wa Soko au tofauti. kwani katika Kanuni hizi zimetoa tafsiri ya Mkuu wa Soko tu.

3. Kamati inashauri kuwekwa kwa tafsiri ya neno **"Eneo la Biashara"** kwani neno hilo ndani ya Kanuni hizi limejitokeza maeneo mengi ili maeneo hayo wajulikane ni yapi ili mtumiaji wa Kanuni hizi asije kuvunja utaratibu,

Vile vile, Mamlaka ndiye yenye uwezo wa kuanzisha na kusimamia masoko kupitia Mkuu wa Soko lakini hakujazungumzwa ni nani atakaeanzisha Eneo ya Biashara. Rejea Kanuni ya 3 na 4. Na upi utaratibu wake ijapokuwa Kanuni ya 26.28,39 30

4. Kamati inashauri katika maneno ya kichwa cha habari ya sehemu ya pili kuongezwa maneno "na maeneo ya biashara" mwishoni mwa kichwa cha habari hicho.

5. Kamati inashauri katika kifungu cha 3 na kwa kuzingatia shughuli za kiuwekezaji Mamlaka ziwe huru kuanzisha masoko na shughuli za kiuwekezaji hata nje ya maeneo yake ya kiutawala ili kwa madhumuni ya kuengeza vyanzo vya mapato kwa Mamlaka hizo.

6. Kanuni ya 5, Kamati inataka kufahamu kwamba Kanuni hii imejielekeza katika **Wajibu wa Mamlaka katika Masoko** lakini hata hivyo ndani ya Kanuni hii kumeguzwa **Maeneo ya Soko au Maeneo ya Biashara.**

7. Kamati inashauri katika Kanuni ya 6, kufanyiwa marekebishwa kama ifuatavyo:

    d) Aya ya (a) kufutwa.

    e) Aya ya (b) kuingiza maneno **"yanayokiuka taratibu za Kanuni hizi"** baina ya neno **"Kamati"** na **"juu".**

f) Aya ya (d) kuongeza maneno **“kwa kuzingatia Masharti ya Sheria”** mwishon mwa aya hii.

8. Kanuni ya 9 Kamati inashauri kurekebishwa kama ifuatavyo:

    a) Aya ya (a) kuingiza neno **“sheria”** baina ya neno **“uchumi”** na **“biashara”**

    b) Aya ya (b) kufuta neno **“mitatu”** na kuweka badala yake neno **“saba”**.

9. Kamati inashauri katika Kanuni 10(b)(ii) kufutwa neno **“na”** liliopo baina ya neno **“ndani”** na **“nje”** na kuweka badala yake maneno **“maeneo ya”.**

10. Kamati inashauri katika Kanuni 12(3)(a) kufutwa aya hiyo. Kwani taratibu hizo zinafuatwa awali kabla hayaajiriwa mtumishi wa umma.

11. Kamati inashauri katika Kanuni ya 13(g) inarekebishwa kwa kuingiza maneno **“kwa mujibu wa Sheria na Kanuni hizi”**.

12. Kamati inataka kujua **“Afisa mapato**” alietajwa katika kanuni ya 13 ni Mamlaka au Soko, kwani majina yote mawili yametumika katika Kanuni hizi mfano katika kanuni ya 13 na 15(1)(g).

13. Kanuni ya 15, Kamati imeona kuna umuhimu wa kuitambia Kamati ndogo ya Jumuiya ya wafanyabiashara. Hivyo inashauri Aya ya **“d”** kuangalia wajumbe wa tatu wa Kamati ya uamuzi ya jumuiya ya wafanya biashara.

14. Kamati inashauri katika kipengele cha Uendeshaji na Usimamizi wa Soko kuwepo na kipengele cha muda na ukomo wa miaka ya kufanya kazi wa kamati hizo ili kuweza kuleta ufanisi mzuri wa masoko hayo.

15. Kanuni ya 20, Kamati inashauri kuingizwa maneno “**ya wingi wa wajumbe”.**

16. Kanuni ya 23, Kamati inashauri kufutwa kwa maneno "**haraka iwezekanavyo baada ya kutambua".**

17. Kanuni ya 24, Kamati inashauri kuwe na utaratibu mzuri watumizi wa maneno kwani katika maneno ya pembeni kumetumiwa neno **"watumishi"** na ndani ya Kanuni neno **"mfanyakazi"** hivyo kutumike neno moja wapo kati ya hayo ndani ya Kanuni hii na maneno ya pembeni.

Aidha, marekebisho hayo yafanyike kila yatapojitokeza maneno kama hayo ndani ya Kanuni hizi.

18. Kanuni ya 27, Kamati inashauri kufutwaa kwa maneno **"regista ya"** na uweka badala yake **"kitabu cha usajili wa".**

19. Kanuni ya 28(d) inarekebishwa kwa kuengezwa maneno **"ya chakula"** baina ya maneno **"biashara"** na **"na ameruhusiwa".**

20. Kanuni ya 31(a), Kamati inashauri kufutwa kwa maneno **"regista ya"** na uweka badala yake "kitabu cha usajili wa"

21. Kanuni ya 32, 34 na 37, Kamati inashauri kuangaliwa upya muda wa ufungajiwa wa masoko

22. Kanuni ya 36, Kamati inataka kufahamu ni lipi "**eneo la wazi**" linalozungumziwa ndani ya Kanuni hizi, kwani ndani ya Kanuni hizi zimeweka "**Maeneo ya Soko** au **Eneo la Biashara**" utaratibu wake.

23. Kanuni ya 39, Kamati inashauri kuingizwa neno **"au"** baina ya neno **"kitanzania**" na **"kifungi"**

24. Kanuni ya 41, Kamati inashauri kufutwa neno **"la"** liliopo baina ya neno **"katika"** na **"soko"**

25. Kanuni ya 41, Kamati inashauri kufutwa neno "**bila ya ruhusa ya Mkuu wa Soko"** yaliopo mwanzoni mwa proviso ya Kanuni hiyo.

26. Kanuni ya 43(2), Kamati inashauri kuingizwa neno **“au”** baina ya neno **“kitanzania” na “kifungi”**

27. Kanuni ya 56(1), Kamati inashauri kufutwa kwa maneno **“sehemu za biashara au sokoni”** na kuweka badala yake maneno **“soko au eneo la biashara isipokuwa”**

28. Kanuni ya 57(a) na (b), Kamati inashauri ziangaliwe upya aya hizo kwani haziko wazi kiuandishi wa sheria. Aidha, aya ya “i”, Kamati inataka kufahamu jee kuna Kanuni inayoweka utaratibu wa uvutaji wa sigara hadharani. Pia, kufutwa na kuandikwa upya neno **“kintaziania”** na kuweka badala yake **“kitanzania”.**

29. Kamati inashauri kanuni ya 60 ifutwe kwa sababu inatoa mianya ya rushwa.

30. Kanuni ya 61, Kamati inashauri kufutwa kwa maneno ya pembeni na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo **“Wajibu wa Mamlaka au Wakala”.** Aidha, Kamati inataka kufahamu ni **wajibu** au ni **majukumu** yaliopo katika Kanuni hii.

31. Kamati inashauri kanuni ya 62 iangaliwe upya kwani kwa ilivyoandikwa inaonekanwa usafi utafanywa mara moja tu kwa siku ilioteuliwa wakati jambo la usafi linapaswa kufanya kila siku ili kuhakikisha masoko yetu yanabakia katika hali ya ubora na kuvutiwa kwa muda mrefu.

32. Kamati inashauri kuwepo na kanuni kwenye Kanuni hizi kitakachoonesha kipengele cha kufanyiwa ukarabati masoko hayo.

33. Kanuni ya 65(2), Kamati inashauri kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo: **“katibu mkuu atasikiliza rufaa hiyo na kutoa uamuzi ndani ya siku saba za kazi kuanzia siku iliyopelekwa rufaa hiyo”.** Aidha, Kamati inataka kufahamu Je, Kanuni hii imezingatia vipi wafanyabiashara ya vyakula vinavyoharibika kwa urahisi.

**Naomba kuwasilisha**

**……………………………………………**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

## 5.6 KIAMBATANISHO NAMBARI 6

## KANUNI ZA KUMALIZA MAKOSA, 2023

Kamati ilipitia Kanuni hizi kwa undani na kukutana na Wadau walioshiriki kutunga hizi pamoja na watumiaji wa Kanuni hizo. Kamati ilibaini changamoto kubwa licha ya kwamba Kanuni hizi zimezingatia utaratibu wa uandishi wa kisheria.

Miongoni mwa changamoto hizo ni kanuni ya 2 inayokuhusu Matumizi ya kanuni, (Application) kanuni imeeleza kwamba itatumika **kwa taasisi zote za "umma" na "binafsi".**

Kimsingi Masharti ya Kanuni hii yanapingana au tuseme yanakinzana na masharti ya kifungu cha matumizi cha *sheria nambari 2 ya 2011,* ambapo kifungu hicho kinaeleza kuwa sheria hiyo ndio itakuwa sheria kiongozi katika masuala yote ya usimamizi wa utumishi wa umma hata kama taasisi ina sheria yake wenyewe.

Mfano katika jadweli la kwanza kipengele cha 11 kinazungumzia kuwa ni kosa kwa muajiri kushindwa kutoa taarifa kwa kamishna juu ya ***kumalizika kwa Mkataba wa Ajira wa Mfanyakazi wa kigeni***.

kimsingi kanuni hiyo inapingana na *kifungu cha 59 cha sheria namba 2 ya 2011* pamoja na *kanuni ya 95 ya kanuni za utumishi za mwaka 2014,* ambapo zote kwa pamoja zinaelekeza kwamba ***ajira ya mtumishi wa kigeni*** itatolewa kwa mujibu wa maelekezo ya ***Katibu Mkuu Kiongozi***. Aidha, kuanza na kumalizika kwa Mkataba wa Mtumishi wa Kigeni taarifa zake zinategemea maelekezo ya Katibu Mkuu Kiongozi.

Hivyo basi, Kanuni hii ya Kumaliza Makosa inatengeneza utaratibu wa kuwa na Mamlaka mbili za adhabu kwa jambo moja (**DOUBLE JOEPARDY).**

Makosa mengine yaliyoainishwa katika kanuni hii, hayawezi kujitokeza katika Utumishi wa Umma kwa mfano kosa katika **Jaduweli la kwanza kipengele cha 2,3,5,6** hayawezi kupatikana katika Utumishi wa Umma. ambapo kosa namba 2 na 3 ajira ya Mtoto Mdogo ambapo katika Utumishi wa Umma anae ajiriwa hulazimika kuwa na **Kitambulisho cha Mzanzibar** ambacho kukipata kwake ni lazima ufikie umri wa utuuzima katika msingi huo hakuna mtoto atakaeajiriwa katika utumishi wa umma asijekuwa na kitambulisho cha mzanzibar ambapo kiutaratibu ili ukipate lazima uwe umetimiza umri wa mtu mzima.

Kamati inashauri kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo:

Neno **Afisa Kazi "maana yake ni Afisa Mkuu wa Kazi Pemba, Maafisa wa Mikoa na Wilaya na inajumuisha Kamishna wa Kazi kama ilivyelezwa chini ya masharti ya Sheria"**

Neno **Afisa Muhasibu** Kamati inaagiza kufutwa neno "au" liliopo baina ya neno **"na"** na **"matumizi".**

Neno **kamishna** Kamati inaagiza kufutwa neno **"sheria"** na kuweka badala yake **"Sheria"**

Kamati inaagiza kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo: **Mkaguzi Kazi "maana yake ni mtu yeyote mwenye haki na wajibu kama ilivyoainishwa chini ya masharti ya Sheria"**

Kanuni ya 5, Kamati inaagiza kufutwa maneno ya pembeni na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo; **"Majukumu ya Afisa Kazi na Mkaguzi Kazi katika Kumaliza Makosa"**

Katika kanuni ya 5 na 6(c), Kamati inataka kufahamu huyu Afisa Uchuguzi ni nani kwani katika tafsiri ya maneno hakufanyiwa tafsiri.

Kamati inataka ufafanuzi wa kanuni ya 7.

Kamati inashauri kuongezwa kwa kanuni 10, ambayo itaweka sharti ya kwamba **“endapo Mtu au Muajiri atashindwa kutekeleza amri ya kumaliza kosa Kamishna anaweza kuchukua hatua za kufungua mashtaka ya jinai dhidi ya Mtu au Muajiri huyo”.**

**Naomba kuwasilisha**

**..............................................**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

## 5.7 KIAMBATANISHO NAMBARI 7

## KANUNI ZA MASUALA YA DIASPORA (USAJILI WA DIASPORA)

Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo ni moja kati Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, iliyoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya **Kanuni 107 ya Kanuni za Kudumu za Baraza Toleo la 2020**.

Aidha, majukumu ya msingi yameelezwa kiujumla katika ***Jaduweli la Kwanza Kipengele cha 1 ndani ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2020.***

Mbali na majukumu mengine yaliyoorodheshwa katika Kanuni hizo. Kamati ina jukumu la kuhakikisha mamlaka waliyoyakasimu kwa Taasisi husika chini ya ***Kifungu cha 79(6) cha Katiba ya Zanzibar 1984,*** yanatumika ipasavyo.

Hapo ndipo ile dhana ya msingi ya kisheria ya inayohitajika ya anayekasimu madaraka anatakiwa kusimamia madaraka hayo **"*Deligation and Supervision".***

Kwa kuzingatia masharti ya ***Sheria nambari 7/1984. kifungu cha 36 na 37,*** Sheria ndogo au Kanuni inakuwa imekamilika kutungwa baada ya kuwekwa saini na aliyekasimiwa Mamlaka hayo pamoja na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Hivyo, Kamati ya Baraza inaweza kutekeleza wajibu wake wa kuzisimamia Kanuni baada ya hatua hiyo kukamilika.

Kamati baada ya kupitia Kanuni hii kwa kina pamoja na kukutana na Wadau, ilibaini kasoro kadhaa miongoni mwa changamoto hizo Kamati ilitoa maelekezo kwa Taasisi husika kwenda kuyafanyia

kazi na hii leo hapa Kamati inatarajia kuyatolea maamuzi kwa yale ambayo wamekwenda kuyafanyia kazi.

Aidha, marekebisho mengine ni pamoja na:

Kanuni imekosa maneno ya pembeni, hivyo, Kamati inashauri kanuni, iwekewe maneno ya pembeni ili iweze kufuata utaratibu wa uandishi wa sheria unaotumika nchini na pia kumsaidia msomaji kwani maneno hayo kumsaidia msomaji kupata urahisi wa rejea.

Kanuni haikuweka Kanuni ya za adhabu kwa mtu anayeuka masharti kwa mtu yaliyowekwa na Kanuni

**SEHEMU YA KWANZA**

1. Kanuni ya 2 inarekebishwa kama ifuatavyo:
    a) kuongezwa tafsiri ya neno jipya "mtoto wa kuasili" kabla ya neno "mtoto wa kulea" na isomeke kama ifuatavyo:
    **Mtoto wa Kuasili: "maana yake ni mtoto aliyefuata utaratibu wa kisheria kutolewa kwenye usimamizi wa wazazi wake wa asili ambao wanaasili ya Zanzibar na kuwa chini ya usimamizi wa Diaspora kwa amri ya mahakama."**

    **b)** Katika tafsiri ya neno "**Ofisi"** Kamati inashauri kuongeza maneno **"kama ilivyoanzishwa kwa kuzingatia masharti ya kifungu cha 4 cha Sheria."** Mwishoni mwa tafsiri ya neno hilo.
    **c)** "**aliyebadilisha utambulisho wake"** kufutwa na kuandikwa upya **"maana yake ni mtu wenye asili ya Zanzibar ambaye alibadilisha utambulisho wake wa asili baada ya kuondoka Zanzibar".**
    **d)** "**Mtegemezi"** Kamati inashauri kufutwa na kuandikwa upya **"maana yake ni mtoto wa kuzaa, kulea au wa kuasili wa Diaspora mwenye asili ya Zanzibar.**

**SEHEMU YA PILI**

Kanuni ya **3(4)** Kamati inashauri kufutwa neno **"mtu"** na kuwekwa badala yake neno **"Diaspora"** kwani kanuni hii inakusudia kuwaondoa katika hatia wana diaspora tu ambao wametoa taarifa zisizo sahihi wakati wa kuomba kusajiliwa.

Kanuni ya **4(C)** Kamati inashauri aya hiyo iangaliwe tena na ni busara kuzingatiwa makosa makubwa ambayo yanahesabika kama ni uhalifu wa kimataifa (***Serious Organize Crime)*** au ***(White Collor Crime).*** kama vile ***makosa ya Dawa za Kulevya, Utakatishaji wa Fedha Haramu na Usafirishaji wa Binadamu.***

*Aidha, hoja ya kuzingatia miezi sita ya kifungo ni suala zaidi la taratibu za kiutumishi.*

Kamati inashauri Kanuni ya 4(d) kuingizwa maneno **"kwa mujibu wa Sheria"** mwishoni mwa aya hiyo ili kuondoa utata kisheria.

Kanuni ya 8(f) kamati inashauri kuongezwa maneno **"kwa kuzingatia masharti ya Sheria"**

Kanuni ya 9(a) kamati inashauri kufutwa neno **"tu"** mwishoni mwa aya hiyo.

Kanuni ya 10 kamati inashauri maneno "cha awali" yatoke kwani yapo mazingira ambayo mtu anaweza kupoteza kitambulisho ambacho si **cha awali** na utaratibu wake haujaelezwa.

Kanuni ya 11(a) kamati inashauri kufutwa neno **"kwa"** liliopo baina ya neno **"kupotelewa"** na **"kitambulisho"** na kuweka badala yake neno **"na"**.

Aidha, neno **"chake"** lifutwe na kuwekwa badala yake neno **"husika"**

Kamati inashauri kuangaliwa upya kanuni ya 15 kwani suala la ulinzi wa taarifa binafsi ni muhimu sana na lisipochukuliwa kwa tahadhari linaweza kuathiri maisha ya mtu binafsi hivyo adhabu ya

shilighi milioni tano ni ndogo kwa kosa la kutumia taarifa binafsi za mtu.

Aidha, kamati inashauri adhabu katika kanuni ya 15 ifuate masharti ya adhabu yaliyopo katika kanuni ya 16,17 na 18.

Kanuni ya 19(2) kuongeza maneno **"na kutoa maamuzi kuhusu rufaa hiyo"** mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo.

**NAOMBA KUWASILISHA**

.....................................

Mwenyekiti,

Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo,

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar

## 5.8 KIAMBATANISHO NAMBARI 8

**KANUNI YA BIDHAA CHAKAVU**

Kwa ujumla, Kamati inapongeza Wizara kwa kuona umuhimu wa hali ya juu kutunga Kanuni ya Bidhaa Chakavu**,** 2023, ambazo zinaendana na hali halisi iliyo sasa.

Kamati itafanya Majumuisho aina mbili ya kwanza ya uwasilishwaji wa nyaraka ambapo michango mengi ya Wajumbe wa Kamati yamo ndani ya waraka huu.

Aidha, mbali na waraka huu Wajumbe wa Kamati watakuwa na fursa ya kuchangia zaidi Kanuni hizi wakati tunapowasilisha waraka huu endapo watakapohitaji kufanya hivyo na yatakuwa miongoni mwa mapendekezo au ushauri wa Kamati.

Kamati baada ya kupitia Kanuni hii kwa kina pamoja na kukutana na Wadau mbali mbali wa Kanuni hizi. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kupitia Kanuni hiyo na kubaini mambo yafuatayo:

Kwanza kabisa, Kamati inaagiza katika kifungu wezeshi cha kanuni hizi kiwekwe wazi ni aya ya ngapi katika kifungu hicho kinatoa uwezo huo.

Katika tafsiri ya maneno baadhi ya maneno hayo yarekebishwe kama ifuatavyo:

Neno **"usafirishaji"** linarekebishwa kwa kuingiza neno **"chakavu"** baina ya neno **"bidhaa**" na **"kutoka**"

Kanuni ya 3(d), Kamati inashauri kufutwa neno **"au"** na kuweka badala yake neno **"na"** mwishoni mwa aya hiyo. Aidha, Kamati inashauri kuangalia tena Aya ya (d) imejirejea mara mbili hivyo aya ya (d) moja kuwa (e).

Kanuni ya 4(3), Kamati inataka kujua ni sababu gani zitakazompelekea Katibu kukataa maombi ya leseni Kamati inashauri **kuwekwa wazi sababu hizo ndani ya kanuni hizi**.

Kanuni ya 6, Kamati inashauri kuwekwa wazi ndani ya Kanuni hizi sababu za **kukubali au kukataa kuishwa kwa lesini.**

Kanuni ya 7(1), Kamati inashauri kuagaliwa suala la kufutwa kwa lesini lisianze mwanzo lije baada ya **kupewa onyo kwanza** na **endapo akirejea tena kosa hilo ndipo apewe adhabu ya kusitisha leseni iyo**.

Aidha, katika Kanuni ya 7(2), Kamati inashauri kuwekwa utaratibu mzuri wa kusikilizwa mmiliki wa leseni.

Aidha, Kamati inashauri kuundwa kwa kamati ndogo ambayo itatekeleza hayo kwa maelekezo ya Katibu

Kanuni ya 10(d), Kamati inashauri kuongezwa neno **"chakavu**" mwishoni mwa aya hiyo.

Kanuni ya 11, Kamati inashauri **kuainishwa sababu za kukataa maombi ya kibali hicho Katibu Mkuu ndani ya kanuni hizi**.

Kanuni ya 12(1)(b), kamati inashauri kufutwa kwa neno "**mkurugnezi"** na kuweka badala yake neno **"mkurugenzi".**

Aidha, Kamati inashauri kuhusu Kamati ya Ukaguzi wa Bidhaa Chakavu, kuangaliwa suala la Muda wa Kamati hiyo uwe miaka 2 au 3.

Kanuni ya 13, Kamati inashauri kuangaliwa upya uandishi wa kanuni hii.

Katika Aya ya (a) Kamati inashauri kama ifuatavyo:

a. Katika (ii)Kufutwa kwa neno **"bidha"** liliopo baina ya neno **"na"** na **"chakuvu"** na kuweka badala yake **"bidhaa"**.

**b.** kuongezwe kwa (iii) na kusomeka kama ifuatavyo: **"kulinda Miundombinu ya Serikali"**

Katika Aya ya (d), Kamati inashauri badala ya Kamati itakagua pawe na Mjumbe ambaye atapewa jukumu la kutoa taarifa kwa

kamati baada ya kukagua. Aidha, neno **"kusafirirshia"** liliopo katika aya hiyo lifutwe na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo **"kusafirishia"**

Katika Aya ya (e) na (f)kamati inashuri neno **"bidha"** lisomeke **"bidhaa"** na kila lilipojitokeza katika Kanuni hizi.

Kamati inataka kufahamu kuna ulazima gani wa kuwepo kwa Kamati wakati wa kusafirisha mzigo hasa bandarini.

Kanuni itambue **Chama cha Jumuiya za Chuma au Bidhaa Chakavu**.

Kanuni ya 16, katika kanuni hii Kamati inashauri kurekebishwa kama ifuatavyo:

Aya ya (a)(i) Kamati inashauri kuongezwa neno **"na"** baina ya neno **"kuwa"** na **"kibali".**

Aya ya (e) kwa kuongeza neno **"au"** mwishoni mwa aya hiyo.

Aidha, Kamati inashauri kuwekwa kwa kiwango cha juu na chini cha faini kwa aliyetenda kosa katika kanuni hiyo.

Kamati 17, kamati inashauri kuwekwa kwa kiwangi halisi cha fedha badala ya kuweka asilimia kumi ya thamani ya mzigo.

Kamati inashauri **"Sehemu ya Tano"** iliopo katika ukurasa **(1013)** isomeke sehemu ya **"Sehemu ya Sita"**

Kanuni ya 21, Kamati inashauri rufaa ipelekwe kwa Waziri kwa mtu asiyeridhika na maamuzi ya Katibu Mkuu.

Kamati inataka kufahamu endapo umekamatwa mzigo utaratibu wa utaifishaji wa mzigo huo utakuwaje.

Kanuni ya 22, Kamati inashauri neno **"shehena"** lifanyiwe tafsiri.

**Naomba kuwasilisha**

……………………………………….

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

## 5.9 KIAMBATANISHO NAMBARI 9

## KANUNI ZA JUMLA ZA MFUKO WA HUDUMA ZA AFYA ZANZIBAR, 2023

Kamati ya Baraza inaweza kutekeleza wajibu wake wa kuzisimamia Kanuni baada ya hatua hiyo kukamilika.

Kamati baada ya kupitia Kanuni hii kwa kina pamoja na kukutana na Wadau, ilibaini kasoro kadhaa miongoni mwa kasoro hizo ni:

Kamati inashauri katika kanuni ya 2 kufanyiwe tafsiri ya neno **"Mgeni"**

Kanuni ya 3(2)(b) inarekebishwa kwa kuingiza neno maneno **"mchangiaji"** baina ya neno **"mwanachama"** na **"waliopo"**

Kanuni ya 3(2)(c) inarekebishwa kwa kuingiza neno maneno **"mchangiaji"** baina ya neno **"mwanachama"** na **"uhusiano"**

**Aidha,** Kamati inashauri utumiaji wa maneno **Mwanachama Mchangiaji na Mwanachama** uangaliwe vyema ndani ya kanuni hizi, kwani maneno haya yasipoangaliwa vyema yanaweza kupoteza maana halisi iliyokusudiwa katika baadhi ya kanuni hizi.

Kanuni ya 3(2)(d) kamati inahitaji ufafanuzi kwani kiuandishi inaonekana kuwa na utata.

Kanuni ya 5 inarekebishwa katika maneno ya pembeni na kusomeka kama ifuatavyo "**usajili wa mtoto wa kuzaa, kulea au kuasili".**

Kanuni ya 5(3) inarekebishwa kwa kuingiza maneno **"mchangiaji"** baina ya neno **"mwanachama"** na **"atamsajili"**

Kanuni ya 5(4) inarekebishwa kwa kuongeza maneno **"na kitambulika kisheria".**

Kanuni ya 8, Kamati inahitaji ufafanuzi zaidi. Aidha, Kuhusu kutambuliwa kwa vitambulisho vya kielektroniki.

kanuni ya 10(c) inarekebishwa kwa kufutwa neno **“na”** na kuweka badala yake **“au”** mwishoni mwa aya hiyo.

kanuni ya 12(a) inarekebishwa kwa kuingiza maneno **“au muajiri”** baina ya neno **“ndugu”** na **“wa”**

kanuni ya 12(c) inarekebishwa kwa kufutwa neno **“na”** na kuweka badala yake neno **“au”** mwishoni mwa aya hiyo.

Kanuni ya 16 Kamati inashauri kufutwa kwa adhabu ya kifungo na badala yake kuwekwa faini kwani dhana hii ipo katika mambo ya Utawala zaidi.

Kanuni ya 18(d) inarekebishwa kwa kufutwa neno “na” na kuweka badala yake neno “au”

Kanuni ya 20(3), Kamati inataka kufahamu na ufafanuzi wa kutosha kuhusu kubadilisha utaratibu wa ngazi za vituo vya utoaji wa huduma za afya kwamba Wiziri au Mfuko ndio unaoweza kubadilisha.

Kanuni ya 21(4), inarekebishwa kwa kufutwa kwa neno “upataji” na kuwekwa badala yake neno “upatikanaji” aidha, kamati inataka ufafanuzi wa kanuni hii kwani imebaini mfuko umepewa mamlaka makubwa.

Kanuni ya 22(1), Kamati inashauri kufutwa kwa neno “itatolea” na kuweka badala yake neno “itatolewa”

Kanuni ya 24(2), Kamati inashauri kuingizwa maneno **“au taasisi”** baina ya neno **“mwanachama”** na **“baada”.** Aidha, marekebisho hayo yafanyike katika mstari wa tatu wa kanuni hiyo**.**

Kanuni ya 24(4), Kamati inataka kufahamu kuhusu muda wa kumuarifu kwa nini haukuainishwa. Aidha, utaratibu wa rufaa upoje endapo hakuridhika na maamuzi hayo**.**

Kanuni ya 25(2), Kamati inashauri kurekebishwa kwa kufutwa kwa neno **“zilizotajwa”** liliopo baina ya neno **“dharura” na “chini”**

Kanuni ya 33(a), Kamati inataka kufahamu rufaa hiyo inaenda kwa nani kiutaratibu iainishwe ndani ya kanuni hii.

Kanuni ya 49(1)(d), Kamati inashauri katika kanuni hiyo mamlaka yabaki kwa Bodi au Mkurugenzi Mkuu na sio kwa Kamati ya Bodi inayohusiana na ukaguzi.

**NAOMBA KUWASILISHA**

.....................................

Mwenyekiti,

Kamati ya Kanuni na Sheria Ndogo,

Baraza la Wawakilishi,

Zanzibar

## 5.10 KIAMBATANISHO NAMBARI 10

## KANUNI YA KUCHUA WANAFUNZI WA VITENDO

Kamati ilipitia Kanuni hizi kwa undani pamoja na kukutana na Wadau walioshiriki kutunga na watumiaji wa Kanuni hizo na kubaini changamoto kadhaa licha ya kwamba Kanuni hizi zimezingatia utaratibu wa uandishi wa kisheria. Kwa kuwa Kamati hii inajukumu la kuhakikisha changamoto hizo zinarekebishwa ili kuwa na Kanuni.

Kanuni ya1, Kamati inashauri kuongezwe maneno **"na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali"** kwani ni matakwa ya uandishi wa kanuni kwa mujibu wa sheria ya tafsiri ya sheria.

Kanuni ya 4(2), katika Aya(a), Kamati inashauri neno **"au"** kufutwa na badala yake liandikwe katika Aya ya **"b"** ya kanuni ndogo hiyo. Ili iendane na utaratibu wa uandishi.

Kamati inataka ufafanuzi wa kanuni ya 4(3) ili kujiridhisha.

Kanuni ya 5(2), Kamati inashauri kuwekwa maneno **"maombi hayo"** mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo.

Kanuni ya 5(3), Kamati inashauri kufutwa neno **"wake"** mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo.

Kanuni ya 6(1), Kamati inashauri kufutwa kwa namba **"5"** iliopo baina ya **"ya"** na **"ya"** na kuwekwa badala yake **5(1).**

Kanuni ya 7(1), Kamati inataka kufahamu ni wanafunzi wa aina gani ambao wanaotakiwa kulipwa posho.

Kanuni ya 8(a), Kamati inataka ufafanuzi wa aya hiyo nini wamekusudia.

Kanuni ya 10, Kamati inashauri kufutwa neno **"madktari"** na kuweka badala yake neno **"madaktari"**

Aidha, Kamati inataka kuelewa kwa jee ilipotungwa kanuni hizi zilizingatia Sheria ya ZSSF yao la kumia kazini namna gani imetambua haki za wanafunzi wa vitendo wamezingatiwaje.

**Naomba kuwasilisha**

**.............................................**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

## 5.11 KIAMBATANISHO NAMBARI 11

## KANUNI ZA UTOAJI VIBALI KWA MAFUNDI WA UMEME,2023

Kamati ilipitia kanuni hizi kwa undani pamoja na kukutana na Wadau walioshiriki kutunga kanuni hizo na kubaini kasoro kadhaa licha ya kwamba kanuni hizi zimezingatia utaratibu wa uandishi wa kisheria.

Kwa kuwa Kamati hii inajukumu la kuhakikisha kasoro hizo zinarekebishwa ili kuwa na kanuni zilizobora.

Hivyo basi, Kamati imebaini yafuatayo kwa ujumla:

- Kuna baadhi ya maeneo ambayo Kamati inahitaji ufafanuzi.
- Kuna baadhi ya maeneo ambayo Kamati imetoa ushauri na mapendekezo.

Kwa mantiki hiyo kanuni zifuatazo zimeguswa kama ifuatavyo:

- Kanuni 2, Kamati ilitaka kupatiwa ufafanuzi zaidi wa baadhi ya maneno yafuatayo:
    - **“Kazi Maalum”**,
    - **“Mafundi Umeme” na**
    - **“Baraza la Taifa la Elimu ya Ufundi (NACTE)”.**
- Kanuni ya 3(3), Kamati inataka kufahamu na kupata ufafanuzi kuhusu maneno **“miezi isiyozidi mitatu”** inakusudia nini?

  Jee iwapo zaidi ya miezi mitatu nini kinafanyika?
- Kamati inapendekeza kanuni ya 3(5) kufuta neno “ya” liliopo baina ya neno **“faini”** na **“isiyopungua”**
- Kamati inaagiza Kanuni ya 4(2)(e) kuangaliwa tena kwani haipo wazi. Aidha, inaitaka Mamlaka kuhakikisha

viambatanisho vyote vinavyohitajika kuambatanishwa na fomu A ya Jadweli la kwanza la kanuni hizi, viainishwe ili kuondoa utata wa kisheria kwa muombaji na kuepusha Mamlaka kutumia madaraka nje ya mipaka ya Sheria.

- Kamati inashauri Kanuni ya 6(2) kufutwa maneno **"kwa kuongezea katika vigezo vilivyoainishwa katika Kanuni hizi na kwa matakwa ya Mamlaka"** na kuweka badala yake maneno **"kwa kuzingatia masharti yaliwekwa katika kanuni ndogo ya (1) ya kanuni hii Mamlaka inaweza kumfanyia majaribio ya maandishi, mdomo na vitendo muombaji**.

- Kamati inashauri Kanuni ya 7(1) kufutwa na kuandikwa upya "**Mamlaka itahakiki uhalali wa taarifa zilizomo na kuamua kukubali ombi la kutoa kibali au kukataa la muombaji.**

- Kamati inashauri maneno ya pembeni ya kanuni ya 10, kufutwa na kuandikwa upya kama ifuatavyo:

    **"muda wa uhalali wa kibali"**

- Kamati inashauri kuangaliwa umuhimu wa uwepo wa **"kibali cha muda mfupi"** katika kanuni ya 12, kwa wala wanaotaka kufanya maomb ya kazi za muda tu ambao watakuwepo nchini.

- Kamati inashauri kuandikwa kanuni mpya ambayo itaweka katazo la ***Mpewa kibali hatoruhusiwa kuhaulisha kibali chake mtu mwengine yeyote alichopewa na Mamlaka***."

**Naomba kuwasilisha**

**..........................................**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

## 5.12 KIAMBATANISHO NAMBARI 12

## KANUNI ZA MAONESHO NA MATAMASHA YA BIASHARA YA 2023,

Kamati inapongeza Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda kwa kuona kwamba kuna umuhimu wa kuanzisha ***Kanuni za Maonesho na Matamasha ya Biashara ya 2023***, ilioanzishwa chini ya kifungu 54(1) cha Sheria nambari 14 ya mwaka 2013.

Kanuni hizi kwa kiasi kikubwa zimezingatia utaratibu wa uandishi wa kisheria licha ya kwamba kuna kasoro zilizojitokeza.

Kamati hii inajukumu la kuhakikisha kasoro hizo zinarekebishwa ili kuwa na kanuni iliyobora na hapo ndipo uwepo wa dhana ya kukasimu madaraka inatekelezwa kwa vitendo.

Kimsingi, Utaratibu wa kutunga Kanuni upo kisheria jambo la kuzingatia Kanuni yoyote inayotungwa itokane na Sheria na anayetunga awe amepewa Mamlaka hayo na Sheria husika, ni lazima kiwepo kifungu wezeshi (enable provision) kinachotoa maelekezo ya kutungwa kwa Kanuni na kutoa Mamlaka kwa mtunzi wa Kanuni. Bila ya kutimizwa kwa masharti hayo Kanuni inayotungwa huwa ni **batili tokea awali (void ab initio).**

Kamati imebaini kwamba kanuni hii imeende nje ya mipaka yake hivyo inataka kufahamu uwezo walioutumia Wizara ya Biashara kutunga kanuni hizi, kwani:

Kwa mujibu wa Sheria Kuanzisha Ofisi ya Mufti namba 4 ya mwaka 2021, chini ya kifungu cha 4(j), kifungu cha 37 na kifungu cha 52(2) (b).

Mamlaka ya Waziri anayesimamia Ofisi ya Mufti ndiye mwenye dhamana ya kutunga ***kanuni inayohusiana na uratibu wa sherehe za kidini*** ambapo Kanuni ya Maonesho na Matamasha

imeingilia uwezo huo, ambapo kiutaratibu Kanuni hiyo haiwezi kuandaa utaratibu unaotekelezwa kupitia sheria nyengine.

Aidha, Kanuni hizi pia, zimeenda kuingilia Sheria ya Baraza la Sanaa nambari 7 ya mwaka 2015 chini ya uwezo waliopewa katika kifungu cha 29(b) ya ***Kuratibu matamasha ya kiutamaduni na kushajihisha kutunzwa kwa utamaduni katika ngazi za Wilaya.***

Kwa mantiki hiyo, ***Kanuni za Maonesho na Matamasha ya Biashara ya 2023,*** haiwezi kukiuka sheria inayohusiana na utamaduni,

Hivyo, Kamati inahitaji majadiliano ya hoja hizi zilizojitokeza ili kuweza kuendelea na majukumu yake ya msingi ya kufanya Majumuisho na Wizara husika.

**Naomba kuwasilisha**

……………………………………….

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

19 Julai, 2024.

## 5.13 KIAMBATANISHO NAMBARI 13

## KANUNI ZA USALAMA WA MAZAO YA CHAKULA

Kamati ya Kanuni na Sheria ndogo ni moja kati Kamati za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, iliyoanzishwa kwa mujibu wa masharti ya **Kanuni za Kudumu za Baraza Toleo la 2024**.

Aidha, majukumu ya msingi yameelezwa kiujumla katika ***Jaduweli la Kwanza Kipengele cha 1 ndani ya Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi Toleo la mwaka 2024.***

Mbali na majukumu mengine yaliyoorodheshwa katika Kanuni hizo. Kamati ina jukumu la kuhakikisha mamlaka waliyoyakasimu kwa Taasisi husika chini ya ***Kifungu cha 79(6) cha Katiba ya Zanzibar 1984,*** yanatumika ipasavyo.

Hapo ndipo ile dhana ya msingi ya kisheria ya inayohitajika ya anayekasimu madaraka anatakiwa kusimamia madaraka hayo **"*Deligation and Supervision*".**

Kwa kuzingatia masharti ya ***Sheria nambari 7/1984. kifungu cha 36 na 37,*** Sheria ndogo au Kanuni inakuwa imekamilika kutungwa baada ya kuwekwa saini na aliyekasimiwa Mamlaka hayo pamoja na kutangazwa katika Gazeti Rasmi la Serikali.

Hivyo basi, Kamati hii inaweza kutekeleza wajibu wake wa kuzisimamia Kanuni baada ya hatua hizo kukamilika.

Kamati ilipitia Kanuni hizi kwa undani pamoja na kukutana na Wadau walioshiriki kutunga na watumiaji wa Kanuni hizo na kubaini changamoto kadhaa licha ya kwamba Kanuni hizi zimezingatia utaratibu wa uandishi wa kisheria.

Kwa kuwa Kamati hii inajukumu la kuhakikisha changamoto hizo zinarekebishwa ili kuwa na kanuni zilizobora. Hivyo Kamati imependekeza yafuatayo kwa ujumla:

Kanuni ya 2 (1), Waziri aongeze zao la mpunga katika jadweli la kwanza ninaloonesha orodha ya mazao chini ya kanuni hizi.

Kamati inashauri katika kanuni ya 4(1)(b) kuongezwa maneno "**na udhibiti wa viatilifu hivyo baada ya matumizi."** Mwishoni mwa aya hiyo.

Kanuni ya 6(g) Kamati inashauri kufutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo: **"Kukagua mazao yenye viashiria vya sumu kuvu au yaliyoripotiwa kuwa na sumu kabla ya kutumika au kuchakatwa".**

Aidha, Kamati inashauri kuongezwa kwa aya mbili mpya ambayo itaweka utaratibu wa ukaguzi wa wafanyabiashara.

**"(h) kuanzisha kitengo mahsusi cha ukaguzi wa viuatilifu vya wafanya biashara; na**

**(i) kuweka utaratibu wa fidia za gharama za uzalishaji kwa mkulima atakaetoa taarifa za sumu kuvu katika mazao yake na ikathibitika."**

Kanuni ya 7(2), Kamati inashauri kuingizwa maneno **"au bwana shamba wa eneo husika"** mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo.

Kanuni ya 7(3), Kamati inashauri kuingizwa maneno **"au bwana shamba wa eneo"** baina ya neno **"Wilaya"** na **"husika".**

Kanuni ya 7(4), Kamati inashauri kuingizwa maneno **"au bwana shamba wa eneo husika"** baina ya neno **"Wilaya"** na **"ametenda".**

Kamati inashauri kuongezwa maneno **"na Afisa huyo anaweza kutoa ruhusa ya uvunaji kwa kuzingatia soko na mahitaji ya zao husika.**

Kanuni ya 7(4) kamati inashauri kuongezwa maneno “na akipatikana na hatia atachukuliwa hatua kwa kuzingatia masharti ya kanuni hizi. Aidha, marekebisho hayo yatafanyika kila yatakapojitokeza maneno hayo ndani ya kanuni hizi kama 8(3),9(3), 10(3), 11(3) na 12(3) na nyenginezo.

Kanuni ya13, Kamati inashauri kanuni kuandikwa upya kwa kuweka wajibu wa wizara kuainisha vigezo na masharti ya vyombo vya usafiri vitakavyotumika kusafirishia mazao.

Kanuni ya 15(1)(a) Kamati inashauri kuongeza maneno **“Afisa Kilimo Wilaya au Bwana Shamba wa Shehia husika**” mwishoni mwa aya hiyo.

Kamati inashauri aya ya 15(1)(b) ifutwe. Aidha, kuwekwe utaratibu wa kuteketeza mazao hayo yenye sumu kuvu. Vile vile, kamati inataka kufahamu utaratibu wa mazao yanayotoka nje ya zanzibar ukoje.

Vile vile, Kamati inashauri kuwekwe kanuni itakayoweza kudhibiti sumu kuvu pamoja na kuwekwa utaratibu mzuri wa kudhibiti sumu kuvu kwa mazao yanayotoka nje ya Zanzibar.

Kanuni ya 15(3), Kamati inashauri maneno Mamlaka husika yawekwe wazi ni ipi imekusudiwa ndani ya Kanuni hii. Aidha, marekebisho hayo yafanyike kila yanapojitikeza maneno hayo ndani ya Kanuni hizi.

Kanuni ya 17, kamati inashauri kufutwa maneno **“mkurugenzi”** na kuweka badala yake **“Afisa Kilimo wa Wilaya”** sababu kila wilaya ina afisa wa kilimo. Aaidha, tumeiwekea ujinai isipotekelezwa hivyo tunatakiwa kuwekea urahisi wa kutekelzwa (compliance). Pia, idadi ya wakulima ni kubwa kuhudumiwa na mkurugenzi mmoja nchi nzima, visiwa vyetu ni Unguja na Pemba kumtoa mtu sehemu moja kwa kufata huduma hiyo wizarani ni usumbufu na inaweza kupelekea kutotiiwa kwa sheria hiyo.

Kuongezwa kanuni ndogo ya 2 mpya na kusomeka kama ifuatavyo: **"Maafisa wa Kilimo wa Wilaya atatoa taarifa za usajili wa wakulima kwa kwa Mkurugenzi".**

Aidha, kuongezwa kanuni ndogo ya 3 ambayo itaonesha **Vigezo Vya Usajili wa Mkulima.**

Kanuni ya ndogo ya 2 kuwa ya 4.

Kanuni ya 18, Kamati inashauri kurekebishwa kwa kufutwa neno **"Mkurugenzi"** na kuwekwa badala yake **"Afisa wa Kilimo wa Wilaya**" mwanzoni mwa kanuni hiyo.

Aidha, kanuni ya 18(2) neno **"Mkurugenzi"** hilo pia litafutwa na kuwekwa**"Afisa wa Kilimo wa Wilaya**"

Aidha, kuwekwe kanuni ndogo ya 3 mpya ambayo itaonesha mazingira ambayo yanaelezea; **"iwapo Mkulima anayeomba kusajiliwa hajatimiza vigezo vya kusajiliwa, Afisa wa Kilimo wa Wilaya atamuelekeza kwenda kukamilisha vigezo hiyo."**

Kanuni ya 18(2) kuwa 18(4) na inafutwa na kuandikwa upya na kusomeka kama ifuatavyo;

**"endapo Afisa wa Kilimo wa Wilaya atakataa ombi la usajili la muombaji baada ya kushindwa kukamilisha vigezo vya usajili wa mkulima, atamuarifu muombaji kwa maandishi na sababu za kukataa huko."**

Kamati inashauri kuongezwa Kanuni 18(5) mpya na kusomeka kama ifuatavyo; **"endapo ombi la kusajiliwa limekataliwa muombaji anaweza kukata rufaa kwa mkurugenzi ndani ya siku kumi na nne za kazi na mkurugenzi anatakiwa kuitolea uamuzi rufaa hiyo ndani ya siku kumi nan ne za kazi tokea kupokea rufaa hiyo."**

Kamati inashauri kuongezwa Kanuni 18(6) mpya na kusomeka kama ifuatavyo; **Rufaa kutoka kwa mkurugenzi itawasilishwa kwa waziri ndani ya siku kumi nan ne za kazi na waziri atatakiwa kuitolea uamuzi rufaa hiyo.**

kanuni ya 20(1) inarekebishwa kwa kufutwa maneno “litatunzwa na mkurugenzi” na kuweka badala yake maneno **“litakuwa chini ya Usimamizi wa Mkurugenzi”**

Kanuni ya 20(2)(c) inarekebishwa kwa kuingiza maneno **“au Kitambulisho cha Mtanzania (NIDA)”**

Kamati inashauri Kanuni ya 20(2)(g) inarekebishwa kwa kuongeza maneno **“kwa mujibu wa Sheria na kanuni hizi”** mwishoni mwa aya hiyo.

Kanuni ya 21 kamati inashauri kurekebishwa kwa kufutwa maneno **“iliyotolewa atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani”** na kuwekwa badala yake maneno **“haikuainishwa na akipatikana na hatia”** baina ya neno **“maalum”** na **“atalipa”.**

**MAONI YA JUMLA**

Kanuni ya 7, kamati inashauri kuwekwa utaratibu wa maombi ya ruhusa na muda wa kujibiwa maombi hayo uweke wazi, ili kuondosha au kupunguza urasimu kwa wakulima na wafanya biashara.

Kamati unashauri kuangaliwa kwa upande wa mfanyabiashara. Aidha, Adhabu na Utaratibu wake uwekwe vyema ndani ya kanuni hizi. Rejea kanuni ya 15 na Sehemu ya Pili maneno ya Kichwa cha Habari zimetambua wafanyabiashara.na wakulima.

Mwisho kabisa;

Kamati inashauri kuangaliwa vyema kanuni ya kudhibiti na uingizaji wa sumu kuvu katika bidhaa za chakula 2023 inayotokana na Sheria nambari 2 ya 2006, kamba hazigongani na kanuni hizi ili kuweza kudhibiti muingiliano wa kanuni hizo na kuweza kuwa kanuni zilizo bora zaidi.

**Naomba kuwasilisha**

**……………………………………….**

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**

## 5.14 KIAMBATANISHO NAMBARI 14

## KANUNI ZA UMMA (USIMAMIZI WA UHAMISHO KWA WATUMISHI WA UMMA WANAOHAMISHWA KIKAZI NJE YA UTUMISHI WA ZANZIBAR), 2024.

Kamati ilipitia Kanuni hizi kwa undani pamoja na kukutana na Wadau walioshiriki kutunga na watumiaji wa Kanuni hizo na kubaini changamoto kadhaa licha ya kwamba Kanuni hizi zimezingatia utaratibu wa uandishi wa kisheria.

Kwa kuwa Kamati hii inajukumu la kuhakikisha changamoto hizo zinarekebishwa ili kuwa na kanuni zilizobora. Hivyo basi, Kamati imependekeza yafuatayo kwa ujumla:

- kanuni ya 2(a) kuingizwa maneno mapya **"muungano wa"** baina ya maneno **"ya"** na **"Tanzania"**.

  Aidha, katika kanuni hiyo Kamati pia inatendekeza kuangaliwa upya neno "**inajumuisha"** katika kanuni hii kuwepo kwake ni utata kisheria.

- Kamati inapendekeza kanuni ya 3 kufanyiwa marekebisho kama ifuatavyo:

  c) Katika ufanunuzi wa neno **"Mamlaka ya usimamizi wa Nidhamu"** kufutwa kwa maneno **"ya utumishi wa Umma**" baina ya neno **"Sheria"** na **"au".**

  d) Katika ufanunuzi wa neno "**Nje ya utumishi wa umma"** lisomeke "**Uhamisho nje ya utumishi wa umma"**.

- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 8 kufutwa kwa neno **"kuathiri"** liliyopo baina ya maneno "**Bila ya"** na "**masharti"** na kuwekwa badala yake neno **"kujali".**

- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 10(2) kufutwa kwa neno **“mtumishi”** liliyopo baina maneno **“mtumishi”** na **“wa umma”.**

- Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni ya 13 kama ifuatavyo:

  c) Kanuni ya 13(4) inafanyiwa marekebisho kwa:

    iii. kufutwa neno **“yeyote**” liliyopo baina maneno **“umma**” na **“ambaye”.** na

    iv. kufutwa maneno **“ambayo hatozingatiwa katika utumishi wake”** yaliyopo baada ya maneno **“sekta binafsi”.**

  d) Kanuni ya 13(5) inafanyiwa marekebisho kwa kufutwa kanuni ndogo hiyo.

- Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni ya 16(3) kama ifuatavyo:

  c) Kwa kufutwa maneno **“nyongeza ya mshahara au**” yaliyopo baina ya maneno **“kumpatia**” na **“bonasi”.**

  d) Kwa kufutwa neno **“ummt”** na kuwekwa badala yake neno **“umma”.**

- Kamati inapendekeza katika kanuni ya 21 kufutwa kwa maneno **“sekta binafsi”** yaliyopo baina maneno **“sekta binafsi”** na **“itakuwa”.**

- Kamati inapendekeza kufanyiwa marekebisho kanuni ya 25(4) kama ifuatavyo:

  c) Kwa kufutwa maneno **“mma**” yaliyopo baina ya maneno **“utumishi wa**” na **“atakuwa”** na kuwekwa badala yake neno **“umma”.**

d) Kwa kufutwa neno **“mma” liliyopo mwishoni mwa kanuni ndogo hiyo** na kuwekwa badala yake neno **“umma”.**

**MAONI YA JUMLA YA KAMATI**

i. Kamati inapendekeza neno **“masuala ya kiutumishi**” linalopatikana katika kanuni ya 3 ya Kanuni hizo lifanyiwe tafsiri upya kwani masuala ya kiutumishi hayaishii tu kama yalivyoainishwa katika kanuni bali yapo mengine yanayohitajika kuwepo katika neno hilo la ufanunuzi.

ii. Kamati inaitaka Wizara kuangalia vizuri mantiki iliyokusudiwa katika kanuni ya 13(4) na 23 kwa mtumishi wa umma atakaekataa kwa makusudi matakwa ya Serikali, je masharti ya kanuni hiyo hayapingani na Kanuni ya 63 ya utumishi ya mwaka 2014.

Je, likizo bila ya malipo huwa inatolewa na muajiri au mtumishi lazima aiombe. Kwa kuzingatia masharti ya kanuni ya 63 ya mwaka 2014 likizo bila ya malipo inamuda maalum?

Je, likizo bila ya malipo inayotolewa na kanuni hizi ina muda gani?

iii. Kamati inapendekeza katika kanuni ya 19 maneno **“pande zote mbili”** zikafafanuliwe vizuri ili zijulikanwe kwa urahisi.

iv. Kamati inapendekeza maneno **“Mkataba Maalum”** na **“Mkataba Mama”** yaliotumika katika Kanuni hizi kufanyiwa tafsiri.

v. Kamati inapendekeza katika kanuni ya 3 katika neno **“Mkuu wa Taasisi”** kufutwa kwa maneno “**Katibu Mkuu”** ambapo neno hilo “**Katibu Mkuu”** inashauriwa liwe na tafsiri yake inayojitegemea.

vi. Kamati inashauri katika matumizi ya maneno bila ya kuathiri na bila ya kujali yaangaliwe upya kwani kutumika kwake bila ya umakini kutapelekea kutoteza dhana zima ya kanuni ilivyokusudiwa ndani ya kanuni hizi.

**Naomba kuwasilisha**

……………………………………………

**MWENYEKITI**

**KAMATI YA KANUNI NA SHERIA NDOGO**

**BARAZA LA WAWAKILISHI**

**ZANZIBAR**